دروس
شَهْرِ رَمَضَانَ

DARASA ZA
MWEZI WA RAMADHANI

Mwandishi:
Abu Halima Arafat
Simu: 0715263253.

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila sifa njema anastahiki Allaah ambaye ameufadhilisha mwezi wa ramadhani kwa kuiteremsha ndani yake Qur'an hali ya kuwa ni uwongofu kwa watu. Swala na salamu zimuendee Mtume wetu Muhammad ambaye amesema:

«إِذَا جَاءَ رَمَضَانُ فُتِّحَتْ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ، وَغُلِّقَتْ أَبْوَابُ النَّارِ، وَصُفِّدَتِ الشَّيَاطِينُ»

"Inapoingia Ramadhani milango ya pepo inafunguliwa, na milango ya moto inafungwa, na hufungiwa mashetani"[1].

Ndugu msomaji, darasa hizi ni mkusanyiko wa Makala zangu mbalimbali kuhusiana na mwezi mtukufu wa Ramadhani nikielezea mambo na hukumu mbalimbali zinazofungamana na mwezi huo, Makala hizi niliandika mwaka (1441h) hijria.

Sababu ya kuzikusanya pamoja Makala hizi ni kutokana na rai za baadhi ya ndugu zangu wakiniomba niandike kitabu kuhusiana na mambo yanayohusu mwezi huu mtukufu, nikajibu matakwa yao na kukubali rai yao baada ya kumuomba Allaah aniruzuku katika hilo Ikhlaas na Taufiq katika kutimiza muradi wangu.

Nimejaribu kupangilia kazi yangu hii kwa mtindo wa baadhi ya vitabu vilivyoandikwa kuhusiana na **Darasa za mwezi wa Ramadhani**, ikawa jumla ya darasa zote ni saba.

Pamoja na hayo, nimeongeza mambo mengi ambayo hayakuwepo katika Makala zilizotangulia, pia nimebadili muundo wa uandishi kwa kutaja asili ya maneno (kwa yake ya kiarabu) kasha kufuatishia tarjama yake, nikitaraji katika hilo kunufaisha kwa watu wenye kujuwa lugha ya kiarabu, isipokuwa sehemu ya (Tanbih) ambayo iko mwishoni mwa kitabu nimefupilizika kwa kutaja mambo mbalimbali kwa tarjama kwa ajili ya kufupisha kalamu.

Kadhaalika nimejitahidi kuepuka kauli zenye kutatiza, kwani walengwa wa kwanza katika Makala zetu hizi ni watu wenye mustawa wa kawaida.

Allaah amlipe kheri kila aliyeshiriki kutimiza makusudiwa haya, na pia ampe jazaa njema kila atakayediriki ndani yake kosa lolote akanizindua, na Allaah anijaalie kupokea kosa hilo kwa moyo mkunjufu. Allaah ndiye mwenye kuafikisha.

Abu Halima Arafat,
Pongwe Tanga,
Pongwe Tanga,
Tanzania.

1- Muslim (1079).

DARASA YA KWANZA
FUNGA YA MWEZI WA RAMADHANI

1. FADHILA NA UBORA WA MWEZI WA RAMADHANI

«أَتَاكُمْ رَمَضَانُ شَهْرٌ مُبَارَكٌ»

“Imekujieni Ramadhani (nao ni) mwezi wenye kubarikiwa”(2).

Na Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا جَاءَ رَمَضَانُ فُتِّحَتْ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ، وَغُلِّقَتْ أَبْوَابُ النَّارِ، وَصُفِّدَتِ الشَّيَاطِينُ»

“Inapoingia Ramadhani milango ya pepo inafunguliwa, na milango ya moto inafungwa, na mashetani wanafungiwa”(3).

«إِذَا كَانَ أَوَّلُ لَيْلَةٍ مِنْ شَهْرِ رَمَضَانَ صُفِّدَتِ الشَّيَاطِينُ، وَمَرَدَةُ الجِنِّ، وَغُلِّقَتْ أَبْوَابُ النَّارِ، فَلَمْ يُفْتَحْ مِنْهَا بَابٌ، وَفُتِّحَتْ أَبْوَابُ الجَنَّةِ، فَلَمْ يُغْلَقْ مِنْهَا بَابٌ، وَيُنَادِي مُنَادٍ: يَا بَاغِيَ الخَيْرِ أَقْبِلْ، وَيَا بَاغِيَ الشَّرِّ أَقْصِرْ، وَلِلَّهِ عُتَقَاءُ مِنَ النَّارِ، وَذَلكَ كُلُّ لَيْلَةٍ»

“Unapokuwa usiku wa mwanzo wa mwezi wa Ramadhani wanafungwa mashetani na majini wakorofi (waliobobea kwenye uasi), na inafungwa milango ya moto, wala haufunguliwi mlango wowote, na inafunguliwa milango ya pepo, wala haufungwi mlango wowote, na atasema msemaji: Ewe mwenye kutaka kheri njoo, na ewe mwenye kutaka shari jizuie, na ana Allaah watu anaowaacha huru na moto, na hilo ni kila usiku”(4).

2. SAUMU YA RAMADHANI NI MOJA YA NGUZO ZA KIISLAMU

«بُنِيَ الإِسْلاَمُ عَلَى خَمْسٍ شَهَادَةِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ وَالْحَجِّ وَصَوْمِ رَمَضَانَ»

“Umejengwa uislamu juu ya nguzo tano: Kushuhudia kwamba hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki ila Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wake, Kusimamisha swala, Kutoa zaka, Kuhiji na Kufunga Ramadhani”(5).

3. SAUMU YA RAMADHANI INAFUTA MADHAMBI YALIYOPITA

«مَنْ صَامَ رَمَضَانَ، إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا، غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ

“Mwenye kufunga Ramadhani kwa Imani na kutaraji malipo atasamehewa madhambi yake yaliyopita”(6).

2- Sunan Nasaai (2106).
3- Muslim (1079).
4- Sunan Tirmidh (682).
5- Bukhari (8) na Muslim (120).
6- Bukhari (38) na Muslim (759).

4. SAUMU NI KINGA YA MTU KUTOINGIA MOTONI

«الصِّيَامُ جُنَّةٌ، وَحِصْنٌ حَصِينٌ مِنَ النَّارِ»

“Saumu ni kinga, na ni ngome madhubuti (ya kukuzuia) na moto”[7].

5. MALIPO YA MFUNGAJI SIKU YA KIAMA

«إِنَّ فِي الجَنَّةِ بَابًا يُقَالُ لَهُ الرَّيَّانُ، يَدْخُلُ مِنْهُ الصَّائِمُونَ يَوْمَ القِيَامَةِ، لاَ يَدْخُلُ مِنْهُ أَحَدٌ غَيْرُهُمْ... فَإِذَا دَخَلُوا أُغْلِقَ فَلَمْ يَدْخُلْ مِنْهُ أَحَدٌ»

Hakika katika pepo kuna mlango unaitwa Rayyaan, wataingia kwa mlango huo siku ya kiama wafungaji, hatoingia kwa mlango huo mtu yayote asiyekuwa hao… wakishakuingia utafungwa na hatoingia mtu mwingine yeyote”[8].

6. AMEPATA HASARA AMBAYE HAKUSAMEHEWA NDANI YA RAMADHANI

«رَغِمَ أَنْفُ رَجُلٍ دَخَلَ عَلَيْهِ رَمَضَانُ ثُمَّ انْسَلَخَ قَبْلَ أَنْ يُغْفَرَ لَهُ»

“Amepata hasara mtu ambaye imemfikia yeye Ramadhani kisha ikaondoka kabla hajasamehewa”[9].

7. MWEZI WA RAMADHANI HUTHIBITI KWA MAMBO MAWILI, (KUUONA)

«لَا تَصُومُوا حَتَّى تَرَوُا الْهِلَالَ وَلَا تُفْطِرُوا حَتَّى تَرَوْهُ فَإِنْ غُمَّ عَلَيْكُمْ فَاقْدُرُوا لَهُ»

“Msifunge mpaka muuone mwezi mwandamo, na wala msifungue (shawwaal) mpaka muuone (mwezi), na mkizuiliwa (na mawingu n.k) basi ukadirieni (kwa kukamilisha sha’bani siku 30)”[10].

AU KWA KUPEWA HABARI NA MTU: (Muislamu, Baleghe, Mwenye akili, Muadilifu): Kwa hadithi ya Ibn ‘Umara (Allaah amridhie) amesema:

«تَرَاءَى النَّاسُ الهِلالَ، فَأَخْبَرْتُ رَسُوْلَ اللهِ ﷺ أَنِّيْ رَأَيْتُهُ فَصَامَ وأَمَرَ النَّاسَ بِصِيَامِهِ»

“Watu walionyeshana mwezi mwandamo, nikamueleza Mtume ﷺ kwamba mimi nimeuona, (Mtume) akafunga na akaamrisha watu wengine kufunga”[11].

8. HAIFAI KUFUNGA KWA KUITANGULIA RAMADHANI

«لَا تَقَدَّمُوا رَمَضَانَ بِصَوْمِ يَوْمٍ وَلَا يَوْمَيْنِ إِلَّا رَجُلٌ كَانَ يَصُومُ صَوْمَهُ، فَلْيَصُمْ ذَلِكَ اليَوْمَ»

“Msiitangulie Ramadhani kwa kufunga siku moja au mbili, isipokuwa mtu ambaye alikuwa anafunga funga yake[12], basi na afunge siku hiyo”[13.]

7- Sahihil Jaamii (3880).
8- Bukhari (1896) na Muslim (1152).
9- Sunan Tirmidh (3545).
10- Bukhari (1906) na Muslim (2554).
11- Sunan Abi Daud (2342).
12- Anakusudia mtu ambaye ana yeye kawaida ya kufunga siku ya jumatatu, alkhamis n.k.
13- Bukhari (1914) na Muslim (1082).

9. UHARAMU WA KUFUNGA SIKU YA SHAKA

Amesema Mtume ﷺ:

«مَنْ صَامَ الْيَوْمَ الَّذِي يُشَكُّ فِيهِ فَقَدْ عَصَى أَبَا الْقَاسِمِ ﷺ»

“Atakaefunga siku ambayo hutiliwa shaka ndani yake basi amemuasi Abal Qassim (Mtume ﷺ)”[14].

Amesema Imam Nnawawi (Allaah amrehemu):

"قَالَ أَصْحَابُنَا يَوْمُ الشَّكِّ هُوَ يَوْمُ الثَّلَاثِينَ مِنْ شَعْبَانَ"

“Wamesema maulamaa wetu wakubwa (wa kishafi): Siku ya shaka ni siku ya thelathini ya mwezi wa sha’bani”[15].

10. NI NANI INAWAJIBIKA KWAKE SAUMU YA RAMADHANI?

Mtu ambaye anawajibika kufunga ramadhani awe na sifa zifuatazo: Muislamu, Baleghe, Mwenye akili, Mkazi wa mji, Ana uwezo wa kufunga na ameepukana na vizuizi vya kisheria.

Allaah Ta’alaa anasema

﴿ شَهۡرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلۡقُرۡءَانُ هُدٗى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٖ مِّنَ ٱلۡهُدَىٰ وَٱلۡفُرۡقَانِۚ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهۡرَ فَلۡيَصُمۡهُۖ ﴾

“Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur’an hali ya kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi ** Basi atakayeufikia mwezi huo akawa ni mkazi basi na afunge”[16].

Na Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا رَأَيْتُمُ الهِلَالَ فَصُوْمُوا»

“Mtakapo Uona mwezi mwandamo basi fungeni”[17].

Na wamekubaliana waislamu wote juu ya uwajibu wa kufunga saumu ya mwezi wa Ramadhani kwa mtu aliye timiza masharti tuliyotaja.

Ama kafiri haifai kwake kufunga na wala haitasihi funga yake, kwa sababu yeye si katika wanaostahiki kufunga.

Na endapo atasilimu ndani ya mwezi wa Ramadhani si lazima juu yake kufunga masiku yaliyokwisha pita, kwa kauli yake Allaah:

﴿قُل لِّلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ إِن يَنتَهُواْ يُغۡفَرۡ لَهُم مَّا قَدۡ سَلَفَ﴾

“Waambie wale walio kufuru: Wakikoma watasamehewa yaliyo kwisha pita”[18].

14- Sunan Nasaai (2188)
15- Al-Majmuu’ sharhil Muhaddhab (Jz. 6, Uk. 401).
16- Surat Al-Baqara/185.
17- Bukhari (1906) na Muslim (1081).
18- Surat Al-Anfaal/ 38.

Na akisilimu katika mchana wa Ramadhani kutamlazimu yeye kujizuia katika muda uliobaki wa siku hiyo, kwa sababu amekuwa ni miongoni mwa wanaostahiki (kufunga) ndani ya muda wa kufunga.

11. SAUMU YA MTOTO MDOGO NA MWENDA WAZIMU

Ama mtoto mdogo haipasi kwake yeye kufunga mpaka afikie baleghe:

«رُفِعَ الْقَلَمُ عَنْ ثَلَاثٍ: عَنِ النَّائِمِ حَتَّى يَسْتَيْقِظَ، وَعَنِ الصَّبِيِّ حَتَّى يَحْتَلِمَ، وَعَنِ الْمَجْنُونِ حَتَّى يَعْقِلَ»

“Kalamu imenyanyuliwa kwa watu aina tatu: kwa mwenye kulala mpaka atakapoamka, mtoto mdogo mpaka atakapoota ndoto (ya jimai), na mwenda wazimu mpaka atakapopata akili”(19).

Lakini ni wajibu kwa mzazi au mlezi wake kumzowesha mwanae kufunga tangu akiwa mdogo ili iwe ni wepesi kwake atakapofikia utu uzima na huo ndio mwenendo wa wema waliotangulia, walikuwa wanawaamrisha watoto wao kufunga kisha huenda nao misikitini, mmoja wao akilia kwa sababu ya njaa humpatia kitu cha kumpumbaza.

ALAMA ZA BALEGHE

1. Kuteremsha manii kwa kuota ndoto au sababu nyingine.
2. Kuota nywele pembezoni mwa tupu ya mbele (kinena).
3. Kutimiza miaka kumi na tano.

Ama kwa mwanamke kuna alama ya ziada nayo ni:

4. Kupata Hedhi.

Mwanamke akifikia baleghe akaanza kupata Hedhi katika mchana wa Ramadhani hali ya kuwa amefunga, akamilishe siku yake hiyo na hakuna chochote juu yake (hatolipa), na kama hajafunga ajizuie katika muda uliobaki wa siku hiyo kwa sababu ni katika wanaostahiki kufunga, pia hatoilipa siku hiyo kwa sababu yeye hakuwa miongoni mwa wanaostahiki tangu mwanzo wa kufunga (wakati wa alfajri).

2. MWENDA WAZIMU:

Mwenda wazimu ni miongoni mwa watu ambao si wajibu kwao kufunga, kwa sababu hapahesabiwi kwake wema wala uovu wowote, kwa sababu ya kuondokewa kwake na akili, kwa hiyo hawezi kuzingatia ibada wala Nia, na ibada zote huzingatiwa Nia.

Na akiwa anapatwa na wazimu baadhi ya nyakati na muda mwingine humrudia yeye akili zake, basi itamlazimu yeye kufunga wakati wa kurejea kwake akili si pale anapopata wazimu, na endapo asubuhi amenuwia kufunga halafu akapatwa na wazimu katika mchana wa Ramadhani funga yake ni sahihi, mfano wake ni mtu aliyezimia mchana wa Ramadhani kwa ajili ya maradhi au sababu nyingine, kwa sababu alitia nia ya kufunga hali ya kuwa ana akili timamu, kwani hakuna dalili yoyote ya kubatilisha funga yake, hasa ikijulikana kwamba unamtokea yeye wazimu katika baadhi ya muda tu na muda mwingine anakuwa mzima.

19- Ahmad (Jz. 2, hadithi ya 1327). Abu Daud (4399) na wengine.

Na juu ya kufanyia kazi kanuni hii hatolipa masiku ambayo alikuwa amepatwa na wazimu.

Na endapo zimerejea kwake akili katika mchana wa mwezi wa Ramadhani itamlazimu ajizuie muda uliobaki wa siku hiyo kwa sababu amekuwa ni miongoni mwa wanaowajibika kufunga na wala hatolipa siku hiyo, ni sawa na mtoto akipata baleghe au kafiri akisilimu katika mchana wa Ramadhani[20].

[20]- Rejea kitabu [Majaalis Shahri Ramadhani] cha sheikh Ibn Uthaymin (Allaah amrehemu).

DARASA YA PILI
ADABU ZA KUFUNGA

1. MWANZO WA MUDA WA KUFUNGA

Amesema Allaah Ta'alaa:

﴿وَكُلُوا۟ وَٱشْرَبُوا۟ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ ٱلْخَيْطُ ٱلْأَبْيَضُ مِنَ ٱلْخَيْطِ ٱلْأَسْوَدِ مِنَ ٱلْفَجْرِ ۖ ثُمَّ أَتِمُّوا۟ ٱلصِّيَامَ إِلَى ٱلَّيْلِ﴾

"Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri kutoka katika weusi wa usiku. Kisha timizeni saumu mpaka usiku". [Surat Al-Baqara/187].

Na katika sahihi Muslim umewekwa mlango unaosema:

(بَابُ بَيَانِ أَنَّ الدُّخُولَ فِي الصَّوْمِ يَحْصُلُ بِطُلُوعِ الفَجْرِ)

"Huu ni mlango wa kubainisha kwamba kuingia katika saumu kunapatikana kwa kuchomoza alfajiri (ya kweli)".

Na amesema Imam Nnawawi (Allaah amrehemu):

"وَيَدْخُلُ فِي الصَّوْمِ بِطُلُوعِ الْفَجْرِ وَيَخْرُجُ مِنْهُ بِغُرُوبِ الشَّمْسِ"

"Na ataingia (mtu) katika saumu kwa kuchomoza alfajiri (ya kweli) na atatoka (atamaliza) kwa kuzama jua"[21].

2. MWISHO WA KUFUNGA NI KUZAMA KWA JUA

«إِذَا أَقْبَلَ اللَّيْلُ مِنْ هَا هُنَا، وَأَدْبَرَ النَّهَارُ مِنْ هَا هُنَا، وَغَرَبَتِ الشَّمْسُ فَقَدْ أَفْطَرَ الصَّائِمُ»

"Litakapodhihiri giza la usiku kutokea upande huu (mashariki), na ukaondoka mchana upande huu (magharibi) na likazama jua, basi amefuturu mfungaji (umefika muda wake wa kufungua"[22].

Amesema Ibn Hajar (Allaah amrehemu):

"وَفِي حَدِيثَيِ الْبَابِ مِنَ الْفَوَائِدِ بَيَانُ وَقْتِ الصَّوْمِ وَأَنَّ الْغُرُوبَ مَتَى تَحَقَّقَ كَفَى وَفِيهِ إِيمَاءٌ إِلَى الزَّجْرِ عَنْ مُتَابَعَةِ أَهْلِ الْكِتَابِ فَإِنَّهُمْ يُؤَخِّرُونَ الْفِطْرَ عَنِ الْغُرُوبِ"

"Miongoni mwa faida katika hadithi mbili hizi za mlango huu ni kubainisha muda wa saumu na kwamba wakati wowote ikithibiti kuzama kwa jua imetosheleza (ndio mwisho wa kufunga), na kuna ndani yake ishara ya katazo la kuwaiga Ahlul kitaab, kwa sababu wao huchelewesha kufungua baada ya kuzama jua"[23].

3. SUNNA NI KUHARAKISHA KUFUNGUA/KUFUTURU

«لاَ يَزَالُ النَّاسُ بِخَيْرٍ مَا عَجَّلُوا الفِطْرَ»

"Watu hawataacha kuwa katika kheri muda wa kuwa wanaharakisha kufuturu"[24].

21- Al-Majmuu' (Jz. 3, Uk. 303).
22- Bukhari (1954) na Muslim (1100).
23- Fat-hul baari (Jz. 4, Uk. 198)
24- Bukhari (1957) na Muslim (1098).

Amesema Abu Ddardaa (Allaah amridhie)

«ثَلَاثٌ مِنْ أَخْلَاقِ النُّبُوَّةِ: تَعْجِيلُ الْإِفْطَارِ وَتَأْخِيرُ السُّحُورِ وَوَضْعُ الْيَمِينِ عَلَى الشِّمَالِ فِي الصَّلَاةِ»

“Mambo matatu ni katika tabia za Mitume: Kuharakisha kufuturu, Kucheleweshа kula daku na kuweka mkono wa kulia juu mkono wa kushoto katika swala”[25].

4. SUNNA NI KUANZA KUFUTURU KWA TENDE AU MAJI

Anasema Thabit Al-Bunaani kwamba amemsikia Anas Bin Malik (Allaah amridhie) anasema:

" كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُفْطِرُ عَلَى رُطَبَاتٍ قَبْلَ أَنْ يُصَلِّيَ، فَإِنْ لَمْ تَكُنْ رُطَبَاتٌ فَعَلَى تَمَرَاتٍ، فَإِنْ لَمْ تَكُنْ حَسَا حَسَوَاتٍ مِنْ مَاءٍ"

“Alikuwa Mtume ﷺ anafuturu kwa tende tosa (mbichi) kabla ya kuswali, akikosa anafuturu kwa tende kavu, na akikosa anachota fumba la maji”[26].

5. MALIPO YA KUMFUTURISHA MTU ALIYEFUNGA

«مَنْ فَطَّرَ صَائِمًا كَانَ لَهُ مِثْلُ أَجْرِهِ، غَيْرَ أَنَّهُ لَا يَنْقُصُ مِنْ أَجْرِ الصَّائِمِ شَيْئًا»

“Mwenye kumfuturisha mfungaji atapata yeye mfano wa malipo yake, na hapunguzi katika malipo ya mfungaji huyo chochote”[27].

6. FADHILA ZA KULA DAKU

«تَسَحَّرُوا فَإِنَّ فِي السَّحُورِ بَرَكَةً»

“Kuleni daku kwa sababu katika daku kuna baraka”[28].

Na pia Mtume ﷺ amesema:

"إِنَّ اللهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّوْنَ عَلَى الْمُتَسَحِّرِيْنَ"

“Hakika Allaah na Malaika wake wanawaswalia[29] wenye kula daku”[30].

7. BORA YA DAKU NI TENDE

«نِعْمَ سَحُورُ الْمُؤْمِنِ التَّمْرُ»

“Bora ya daku ya muislamu ni Tende”. [As Sahiha (562)].

8. DAKU NI KITENGANISHI CHA FUNGA YETU NA AHLUL KITAAB

«فَصْلُ مَا بَيْنَ صِيَامِنَا وَصِيَامِ أَهْلِ الْكِتَابِ، أَكْلَةُ السَّحَرِ»

“Kitenganishi baina ya saumu yetu na saumu ya Ahlul kitaab ni kula daku”[31].

25- Majma’u Zzawaaid (Jz. 2, Uk. 105).
26- Sunan Abi Daud (2358).
27- Sunan Abi Daud (807).
28- Bukhari (1923) na Muslim (1095).
29- Allaah anawasifu huko mbinguni na kuwanyanyua daraja na Malaika wanawaombea dua.
30- Sahihi Ttarghiib (1066).
31- Sahihi Muslim (46).

9. MUDA WA DAKU YA MTUME ﷺ NI KARIBU NA ALFAJIRI

Amesema Zaid Bin Thabit (Allaah amridhie):

«تَسَحَّرْنَا مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، ثُمَّ قَامَ إِلَى الصَّلاَةِ»، قُلْتُ: كَمْ كَانَ بَيْنَ الأَذَانِ وَالسَّحُورِ؟ " قَالَ: «قَدْرُ خَمْسِينَ آيَةً»

“Tulikula daku pamoja na Mtume ﷺ, kisha akaondoka kwenda kuswali”, (Anas Bin Malik anasema): nikamuuliza: ulikuwa ni muda gani baina ya adhana (ya pili) na (kumaliza kula) daku? Akasema (Zaid): “kiasi cha kusoma aya hamsini”[32].

10. MWENYE KUSIKIA ADHANA YA PILI AKIWA ANAKULA DAKU

«إذا سَمِعَ أحَدُكُم النِّدَاءَ والإناءُ على يَدِهِ، فَلا يَضَعْهُ حَتَّى يقضِيَ حَاجَتَهُ مِنْهُ»

“Atakaposikia mmoja wenu adhana (ya pili) na hali ya kuwa chombo kipo mkononi mwake, asikiweke chini mpaka akamilishe haja yake katika hicho”[33].

11. WAJIBU WA KULALA NA NIA KATIKA USIKU WA RAMADHANI

«مَنْ لَمْ يُجْمِعِ الصِّيَامَ قَبْلَ الْفَجْرِ، فَلَا صِيَامَ لَهُ»

“Yule ambaye hakunuwia saumu kabla ya alfajri hana funga” [34].

Nia inakuwa moyoni na wala haitamkwi, inatosha kwa muislamu kunuwia usiku wa kwanza kwamba atafunga ramadhani yote, lakini ikitokea ameacha kufunga baadhi ya masiku kwa sababu ya maradhi, safari n.k basi atanuwia upya atapoanza tena kufunga.

12. MTU MWENYE KUSAHAU AKALA MCHANA HALI YA KUWA AMEFUNGA

«إِذَا نَسِيَ فَأَكَلَ وَشَرِبَ، فَلْيُتِمَّ صَوْمَهُ، فَإِنَّمَا أَطْعَمَهُ اللَّهُ وَسَقَاهُ»

“Akisahau (mmoja wenu) akala au akanywa basi akamilishe saumu yake, hakika Allaah ndiye amemlisha na kumnywesha”[35].

13. THAMANI YA HARUFU YA KINYWA CHA MFUNGAJI

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَخُلُوفُ فَمِ الصَّائِمِ أَطْيَبُ عِنْدَ اللَّهِ تَعَالَى مِنْ رِيحِ المِسْكِ»

“Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake, (wallaahi) harufu ya kinywa cha mfungaji inapendeza zaidi mbele ya Allaah Ta’alaa kuliko harufu ya miski”[36].

14. DUA YA MFUNGAJI HAIRUDISWI:

"ثَلَاثُ دَعَوَاتٍ لَا تُرَدّ: دَعْوَةُ الوَالِدِ وَدعْوَةُ الصَّائِمِ وَدَعْوَةُ الْمُسَافِرِ"

“Dua za aina tatu hazikataliwi: Dua ya mzazi, mfungaji na dua ya msafiri”. [As Sahiha (1797)].

32- Bukhari (1921).
33- Sunan Abi Daud (2349).
34- Sunan Abi Daud (2454).
35- Bukhari (1933) na Muslim (1155).
36- Bukhari (1894) na Muslim (1151).

15. DUA BAADA YA KUFUTURU:

«ذَهَبَ الظَّمَأُ وَابْتَلَّت العُرُوقُ وَثَبَتَ الأَجْرُ إِنْ شَاءَ اللهُ»

“Kimeondoka kiu, mishipa imerowa (imelainika) na In Shaa Allaah yamethibiti malipo”[37].

Amesema Imam At-Twiibiy (Allaah amrehemu):

"ذِكْرُ ثُبُوتِ الْأَجْرِ بَعْدَ زَوَالِ التَّعَبِ اسْتِلْذَاذٌ"

“Kutaja kuthibiti kwa malipo baada ya kuondokewa na tabu ni furaha”[38].

16. MFUNGAJI ANA FURAHA MARA MBILI DUNIANI NA AKHERA

«لِلصَّائِمِ فَرْحَتَانِ: فَرْحَةٌ عِنْدَ فِطْرِهِ، وَفَرْحَةٌ عِنْدَ لِقَاءِ رَبِّهِ»

“Ana mfungaji furaha mbili: Furaha wakati wa kufuturu kwake, na Furaha wakati atapokutana na Mola wake Mlezi”[39].

37- Sunan Abi Daud (2357).
38- ‘Aunul ma’buud (Jz. 3, Uk. 346).
39- Muslim (1151).

DARASA YA TATU
MAFUNGU YA WATU KATIKA SAUMU YA RAMADHANI NA KUFUATIWA NA: MAMBO YENYE KUFUNGUZA NA MASHARTI YAKE

Watu katika ibada ya saumu wamegawanyika makundi kumi:

1. FUNGU LA KWANZA: MUISLAMU, BALEGHE, MWENYE AKILI, MKAZI WA MJI, ANAWEZA KUFUNGA, NA AMESALIMIKA NA VIZUIZI

Mtu aliyekamilisha masharti hayo ni wajibu juu yake kufunga Ramadhani katika muda wake, kwa ushahidi kutoka ndani ya Qur'an, Sunnah na Makubaliano ya waislamu juu ya hilo

﴿ شَهۡرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلۡقُرۡءَانُ هُدٗى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٖ مِّنَ ٱلۡهُدَىٰ وَٱلۡفُرۡقَانِۚ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهۡرَ فَلۡيَصُمۡهُۖ ﴾

"Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an hali ya kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi ** Basi atakayeufikia mwezi huo akawa (mkazi) basi na afunge"[40].

Na Mtume ﷺ:

«إِذَا رَأَيْتُمُ الهِلاَلَ فَصُوْمُوا»

"Mtakapo Uona mwezi fungeni"[41].

Na wamekubaliana waislamu wote juu ya uwajibu wa kufunga Ramadhani kwa mtu aliye timiza masharti yaliyo tangulia.

Ama kafiri haifai kwake kufunga na wala haisihi funga yake, kwa sababu yeye si katika wanaostahiki kufunga.

Na endapo akisilimu ndani ya mwezi wa Ramadhani si lazima kwake kufunga masiku yaliyo kwisha pita, kwa kauli ya Allaah:

﴿قُل لِّلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ إِن يَنتَهُواْ يُغۡفَرۡ لَهُم مَّا قَدۡ سَلَفَ﴾

"Waambie wale walio kufuru: Wakikoma watasamehewa yaliyo kwisha pita"[42].

Na akisilimu katika mchana wa Ramadhani kutamlazimu yeye kujizuia masaa (muda) uliobaki wa siku hiyo; kwa sababu amekuwa ni miongoni mwa wanaostahiki ndani ya wakati wa kufunga.

40- Surat Al-Baqara/185.
41- Bukhari (1906) na Muslim (1081).
42- Surat Al-Anfaal/ 38.

2. FUNGU LA PILI: MTOTO MDOGO

Haipasi kwake yeye kufunga mpaka afikie Baleghe, kwa kauli ya Mtume ﷺ:

«رُفِعَ الْقَلَمُ عَنْ ثَلَاثٍ: عَنِ النَّائِمِ حَتَّى يَسْتَيْقِظَ، وَعَنِ الصَّبِيِّ حَتَّى يَحْتَلِمَ، وَعَنِ الْمَجْنُونِ حَتَّى يَعْقِلَ»

“Imenyanyuliwa kalamu kwa (watu) aina tatu: Mwenye kulala mpaka atakapo Amka, Mtoto mdogo mpaka atakapo Ota (ndoto ya jimai), na Mwenda wazimu mpaka atakapopata akili”(43).

Lakini ni wajibu wake mzazi/mlezi kumuamrisha yeye kufunga kwa ajili kumzowesha, ili iwe ni wepesi kwake wakati akifia utu uzima na huo ndio mwenendo wa watu wema walio tangulia, walikuwa wanawaamrisha watoto wao kufunga kisha huenda nao misikitini, mmoja wao akilia kwa sababu ya njaa wanampatia vitu cha kuchezea ili apumbazike navyo, kisha hunyamaza na kuendelea na saumu yake, tafauti na wazazi wengi hivi leo wameghafilika na jambo hili, bali kuna miongoni mwao huwakataza watoto wao wasifunge kabisa kwa hoja kwamba wanawahurumia, hali ya kuwa si sahihi, lakini endapo motto mdogo amefunga kisha ukaona kwake madhara, basi hapana vibaya kumpatia chakula, kwa sababu ni sehemu tu ya kumzowesha si wajibu.

Alama za baleghe kwa mtoto wa kiume

1. Kuteremsha manii kwa ndoto au sababu nyingine.
2. Kuota nywele kwenye kinena pembezoni mwa tupu ya mbele
3. Kutimiza miaka kumi na tano.

   Ama kwa mwanamke kuna ziada ya sifa hizo tatu nayo ni:
4. Kupata Hedhi.

Kwa hiyo mwanamke akifika baleghe halafu ukawa mwanzo wake wa kupata Hedhi ni katika mchana wa Ramadhani hali ya kuwa amefunga basi akamilishe funga yake na hakuna chochote juu yake, lakini akiwa hajafunga ajizuie muda uliobaki wa siku hiyo kwa sababu ni miongoni mwa wanaostahiki kufunga na wala haitolipa, kwa sababu wakati wa uwajibu wa kujizuia (alfajiri ya kweli) yeye hakuwa miongoni mwa wanaostahiki.

3. FUNGU LA TATU: MWENDA WAZIMU

Mwenda wazimu haisihi kwake funga kwa sababu hana akili ya kuweza kuzingatia ibada wala kunuwia, kwa sababu kila ibada haisihi isipokuwa kwa Nia.

Lakini akiwa anapatwa na wazimu baadhi ya wakati na anazinduka (anapata akili) wakati mwingine itamlazimu yeye kufunga wakati wa kuzinduka kwake na si wakati ule alipopata wazimu, na endapo asubuhi amenuwia kufunga halafu akapatwa na wazimu katika mchana wa Ramadhani huyo funga yake ni sahihi haitabatilika ni sawa na mtu aliyezimia mchana wa Ramadhani kwa ajili ya maradhi au sababu nyingine, kwa sababu alitia Nia ya kufunga hali ya kuwa ana akili timamu na hakuna dalili yoyote ya kubatilisha funga yake hasa akijulikana kwamba unamtokea yeye wazimu katika muda fulani na muda mwingine anakuwa mzima.

43- Ahmad (Jz. 2, hadithi ya 1327). Abu Daud (4399) na wengine.

Na kwa kufanyia kazi kanuni hii hatolipa masiku ambayo alikuwa amepatwa na wazimu.

Endapo Mwenda wazimu zimerejea kwake akuli katika mchana wa Ramadhani itamlazimu ajizuie muda uliobaki wa siku hiyo kwa sababu amekuwa ni miongoni mwa wanao wajibika kufunga na wala hatolipa siku hiyo, kama mtoto akipata Baleghe au kafiri akisilimu katika mchana wa Ramadhani.

4. FUNGU LA NNE: MTU MZIMA ASIYEWEZA KUPAMBANUA

Mtu huyu hana uwajibu wa kufunga wala kulisha masikini kwa sababu si Mukallaf (hajakalifishwa na sheria), kwa hiyo ni sawa na mtoto mdogo ambaye hawezi kupambanua kitu chochote. Na akiwa anaweza kupambanua baadhi ya wakati basi ni wajibu wake kufunga wakati wa kujitambua kwake na si wakati wa kuchanganyikiwa, na swala pia ni kama funga itamlazimu kuswali wakati anapopata fahamu. Tunamuomba aturuzuku afya njema.

FUNGU LA TANO: ASIYEWEZA KUFUNGA KABISA

Mfano wake ni mgonjwa ambaye hana matarajio ya kupona, kama vile mgonjwa wa Saratani (Cancer) Ukimwi (Aids) n.k, au mtu mzima ambaye ni tabu kwake kufunga, hao si wajibu kwao kufunga kwa sababu ya kushindwa na badala yake atalisha masikini mmoja kila siku ambayo hakuweza kufunga.

NAMNA YA KULISHA MASIKINI

Mtu amepewa hiyari ya kutoa kila siku nusu ya pishi (pishi ya Mtume ﷺ) kumpatia masikini, hali ya kuwa ni fidia yake kwa kushindwa kufunga saumu ya ramadhani, atatoa chakula kinacholiwa na kupendwa sana katika mji, au kupika chakula cha kuwatosha masikini kwa idadi ya siku ambazo hakufunga, nusu ya pishi ni sawa na kilo moja na robo kwa vipimo vyetu, kwa sababu pishi ya Mtume ﷺ kwa vipimo vya kisasa ni sawa na kilo mbili na nusu kwa sanadi sahihi kutoka kwa Zaid Bin Thabit (Allaah amridhie), kama walivyotusimulia baadhi ya masheikh waliopokezwa kwa sanadi.

6. FUNGU LA SITA: MSAFIRI AMBAYE HAKUSUDII KUKIMBI FUNGA

Kama mtu amesafiri ili aache kufunga kwa hoja kuwa yumo safarini, kufanya hivyo ni haramu kwake na atawajibika kufunga katika hali hiyo. Na yule ambaye hakusudii hivyo basi shreria imempa hiyari baina ya kufunga au kula akiwa safarini na atalipa katika masiku mengine baada ya kurejea, ni sawa umerefuka muda wa safari yake au hapana, kama vile dereva wa ndege, malori au basi za abiria n.k. kwa kauli ya Allaah:

﴿وَمَن كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۚ يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ﴾

“Na mwenye kuwa mgonjwa au yumo safarini basi atimize hesabu katika siku nyingine. Allaah anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito”[44].

Na kauli ya Anas Bin Malik (Allaah amridhie):

[44]- Surat Al-Baqara/185.

«كُنَّا نُسَافِرُ مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَلَمْ يَعِبِ الصَّائِمُ عَلَى المُفْطِرِ، وَلاَ المُفْطِرُ عَلَى الصَّائِمِ»

“Tulikuwa tukisafiri pamoja na Mtume ﷺ wala hakumlaumu mwenye kufunga juu ya aliyekula, wala aliyekula juu ya mwenye kufunga”(45).

Ndiyo maana Abu Said Al-Khudri (Allaah amridhie) akasema kuhusiana na msafiri:

«يَرَوْنَ أَنَّ مَنْ وَجَدَ قُوَّةً فَصَامَ، فَإِنَّ ذَلِكَ حَسَنٌ وَيَرَوْنَ أَنَّ مَنْ وَجَدَ ضَعْفًا، فَأَفْطَرَ فَإِنَّ ذَلِكَ حَسَنٌ»

“(Walikuwa Maswahaba) wanaona yule anayepata nguvu akafunga, basi kufanya hivyo ni vizuri na anayepatwa na kuchoka akala (pia) hivyo ni vizuri”(46).

Na endapo mtu ni dereva na hawezi kufunga pindi akiwa safarini kwa sababu ya joto kali au kuchoka, basi ameruhusiwa kula na atakuja kukamilisha idadi ya siku alizoacha katika siku nyingine, lakini iliyo bora kwake ni kufanya lenye wepesi kwake, na akiweza kuharakisha kutekeleza wajibu na kuondosha dhima basi ni bora zaidi.

Na endapo msafiri ameingia katika mji wake mchana wa Ramadhani hali ya kuwa hakutia nia ya kufunga wakati alipokuwa safarini, basi haitafaa kwake kufunga, kwa sababu nia ya funga ya Ramadhani ni kabla ya kuchomoza alfajiri, kwa hiyo ataendelea kula mchana wa siku hiyo wala hatajizuia, isipokuwa afanye hilo kwa siri na atakuja kulipa siku hiyo baada ya Ramadhani.

FUNGU LA SABA: MGONJWA ANAETARAJIA KUPONA

Mgonjwa wa aina hii ana hali tatu:

Hali ya kwanza:

Ni kuwa hapati tabu yoyote endapo atafunga, katika hali hii ni wajibu wake kufunga kwa sababu hana udhuru wowote kisheria.

Hali ya pili:

Ni kuwa kufunga ni dhiki kwake hata kama hapati madhara, katika hali hii atakula na atakuja kulipa akipona.

Hali ya tatu:

Ni kuwa kufunga kunamletea yeye madhara, hapo ni wajibu wake kula wala haifai kwake kufunga, kwa sababu sheria imekataza mtu kuidhuru nafsi yake.

Allaah anasema:

﴿وَلَا تَقْتُلُوٓاْ أَنفُسَكُمْۚ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا﴾

“Wala msijiue, hakika Allaah ni Mwenye kuwahurumieni”(47).

45- Bukhari (1947) na Muslim (1116).
46- Muslim (1116).
47- Surat An-Nisaa/29.

Kwa maana msifanye jambo la madhara ambalo litapelekea kujiangamiza au kumuangamiza ndugu yako muislamu.

Na Mtume ﷺ amesema:

«وَلِنَفْسِكَ عَلَيْكَ حَقًّا»

“Na nafsi yako ina haki juu yako”(48).

Na miongoni mwa haki zake hiyo nafsi ni kwamba usiitie kwenye madhara, ukafunga huku unapata madhara, hali ya kuwa kuna ruhusa kutoka kwa Allaah ya kula kisha uje kulipa ukipona.

Na akipatwa na maradhi katika mchana wa ramadhani hali ya kuwa amefunga na akashindwa kuendelea na saumu yake, itafaa kwake kufungua (kula) kwa ile ruhusa aliyopewa na sheria.

Lakini kama alikuwa mgonjwa halafu akapona katika mchana wa Ramadhani hali ya kuwa hakufunga (amekula asubuhi) haifai kwake kufunga siku hiyo, kwa sababu funga ya Ramadhani inaanza wakati wa asubuhi na wala hatajizuia na kula, bali atakuja kulipa.

Na endapo Daktari amethibitisha kwamba akifunga atadhurika au kuchelewa kupona, itafaa kwake kula katika mchana wa Ramadhani kwa ajili ya kulinda afya yake na kujichunga na madhara, na ikiwa maradhi hayo ni yale yenye kutarajiwa kupona basi atakuja kulipa siku alizoacha kufunga, ama maradhi yasiyotarajiwa kupona atakula na atatoa fidia kama ilivyotangulia.

FUNGU LA NANE: MWANAMKE MWENYE HEDHI

Ni haramu kwake kufunga na wala haitasihi saumu yake, kwa kauli yake Mtume ﷺ wakati akibainisha upungufu wa dini kwa mwanamke akasema:

«أَلَيْسَ إِذَا حَاضَتْ لَمْ تُصَلِّ وَلَمْ تَصُمْ»

“Je hakuwa anapopata Hedhi haswali wala hafungi?”(49).

Mwanamke akipata hedhi mchana wa Ramadhani hali ya kuwa amefunga hata kama ni kabla ya kuzama jua kwa muda mchache, funga yake imebatilika na atakuja kulipa siku hizo, isipokuwa ikiwa ni funga ya sunna hakuna juu yake wajibu wa kulipa.

Na akitwaharika katika mchana wa Ramadhani haitafaa kwake kufunga siku hiyo kwa muda uliobaki, ataendelea kula katika mchana huo na wala hatajizuia. Lakini akitwaharika usiku katika mwezi wa Ramadhani hata kama ni muda mchache kabla ya kuingia alfajiri ni wajibu juu yake kufunga, kwa sababu hana tena kizuizi, hata kama atachelewa kuoga mpaka asubuhi hapana ubaya na funga yake ni sahihi.

Ama mwanamke mwenye Nifasi hukumu zake ni sawa na mwanamke mwenye Hedhi.

48- Bukhari (1968).

49- Bukhari (304) na Muslim (79).

Kadhaalika ni wajibu kwa mwenye Hedhi au Nifasi kulipa funga tu tafauti na swala, kwa kauli ya Aisha (Allaah amridhie) wakati alipoulizwa, kwa nini mwenye Hedhi analipa funga lakini halipi swala?
Akajibu:

«كَانَ يُصِيبُنَا ذَلِكَ، فَنُؤْمَرُ بِقَضَاءِ الصَّوْمِ، وَلَا نُؤْمَرُ بِقَضَاءِ الصَّلَاةِ»

“Ilikuwa inatupata sisi hiyo (hedhi), tukawa tunaamrishwa kulipa funga wala hatuamrishwi kulipa swala”[50], (anakusudia katika zama za Mtume ﷺ).

FUNGU LA TISA: MANAMKE MWENYE MIMBA AU KUNYONYESHA AKIHOFIA JUU YA NAFSI YAKE AU MWANAE

Endapo mwanamke anahofia kwamba akifunga atachoka sana au mwanawe atakosa maziwa ya kunyonya, basi ameruhusiwa kula katika mchana wa Ramadhani na atakuja kulipa siku zote alizoacha wakati akipata wepesi wa kufanya hivyo, na pia kuna kauli nyingine kinyume na hii ya kwamba atakula na atatoa fidia ya kulisha masikini wala hatolipa saumu, lakini haipasi kwa mwanamke wa kiislamu kufanya hivyo kwa makusudi, hali ya kuwa anaweza kufunga bila madhara yoyote.

FUNGU LA KUMI: MWENYE KUFUNGUA ILI KUKINGA MADHARA KWA MTU MWINGINE

Kama vile kumuokoa mtu anayezama baharini au mwenye kuteketea kwa moto na mfano wake, kama mwokoaji atahitajia kula au kunywa ili atekeleze kazi hiyo, basi atafanya hivyo na atakuja kulipa siku hiyo. Na mfano wake ni mtu mwenye kuhitajia hilo kwa ajili ya kupambana na adui (Jihad), sawa akiwa safarini au katika mji wake atakula mchana wa Ramadhani na atakuja kulipa siku hiyo.

Na endapo mtu baada ya kumalizika Ramadhani hakupona wala hakuweza kufunga mpaka akafa hakuna kitu juu yake, lakini akipona kisha akazembea kwenye kulipa mpaka akafariki, watafunga kwa niaba yake jamaa zake na kama hana ndugu wa karibu au wapo lakini hawataki kufunga basi watoe fidia kwa kulisha masikini.

Na akicheleweshe kulipa bila udhuru wa kisheria mpaka ikafika Ramadhani nyingine, basi ikimalizika atalipa siku alizoacha katika Ramadhani iliyotangulia, pia kuna kauli inasema atalipa masiku ya ramadhani iliyopita pamoja na kutoa fidia kwa kila siku aliyoacha kufunga, kwa sababu ameacha kwa uzembe.

Wabillaahi Ttaufiiq

50- Mukhtasar ya sahihil Bukhari (403) na Muslim (335).

MAMBO SABA YENYE KUFUNGUZA

Allaah anasema:

﴿وَكُلُوا۟ وَٱشْرَبُوا۟ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ ٱلْخَيْطُ ٱلْأَبْيَضُ مِنَ ٱلْخَيْطِ ٱلْأَسْوَدِ مِنَ ٱلْفَجْرِ ۖ ثُمَّ أَتِمُّوا۟ ٱلصِّيَامَ إِلَى ٱلَّيْلِ ۚ﴾

“Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni Saumu mpaka usiku (kuzama kwa jua)”[51].

Katika aya hii tukufu Allaah Ta’alaa ametaja mambo makubwa yenye kufunguza na Mtume ﷺ akatimiza kwa kuyataja mengine kama ilivyothibiti katika hadithi.

JAMBO LA KWANZA: KUFANYA JIMAI (TENDO LA NDOA) MCHANA WA RAMADHANI

Jimai ni kuingiza dhakari kwenye tupu ya mwanamke hata kama hukuteremsha manii. Mtu yeyote aliyefunga akifanya jimai funga yake imebatilika, ni sawa funga ya faradhi au funga ya sunna.

Kisha kama amefanya tendo hilo katika mchana wa Ramadhani hali ya kuwa yeye ni miongoni mwa wanao wajibika kufunga, basi itamlazimu kulipa siku hiyo na kutoa fidia, ambayo ni kuacha huru mtumwa muislamu, akishindwa atafunga miezi miwili mfululizo na kama kuna siku amekula mchana (katika siku za fidia) bila ya udhuru wa kisheria (kama maradhi n.k) basi hesabu haitazingatiwa, badali yake ataanza tena mwanzo, na akishindwa kufunga miezi miwili mfululizo atalisha masikini sitini na tumetangulia kutaja hapo kabla kuhusiana na utaratibu wa kulisha masikini.

Hukumu hii itampata kila muislamu aliyefanya jambo hilo katika mchana wa Ramadhani, ni sawa amemuingilia mwanamme au mwanamke, tupu ya mbele au nyuma, kwa halali au kwa zinaa, hata kama hajateremsha manii, na pia akimuingilia mnyama.

JAMBO LA PILI: KUJITOA MANII (KUJICHUA) KWA MAKUSUDI

Endapo mtu ametokwa na manii kwa kukumbatia, kupiga busu au kujichua kwa mkono au kwa sababu nyingine, funga yake imebatilika kwa sababu hilo ni miongoni mwa matamanio ambayo ni wajibu kwa mfungaji kujiepusha nayo, kwa hadithi inayosema:

«يَتْرُكُ طَعَامَهُ وَشَرَابَهُ وَشَهْوَتَهُ مِنْ أَجْلِي»

“Anaacha chakula chake, kinywaji chake na matamanio yake kwa ajili yangu”[52]

Lakini kama atabusu na kukumbatia bila kuteremsha manii funga yake ni sahihi, na iliyo bora kwa vijana ni kujiepusha nalo.

Ama kuteremsha manii kwa kuota ndoto (mchana wa Ramadhani) au kutafakari (mawazo mbaya) bila kubashiri kitendo jambo hilo halibatilishi saumu, kwa sababu ndoto hutokea bila ya hiyari wala kufikiria, kwa hiyo amesamehewa kwa hadithi:

51- Surat Al-Baqara/187.
52- Bukhari (1894).

«إِنَّ اللَّهَ تَجَاوَزَ عَنْ أُمَّتِي مَا حَدَّثَتْ بِهِ أَنْفُسَهَا، مَا لَمْ تَعْمَلْ أَوْ تَتَكَلَّمْ»

“Allaah ameusamehe Umma wangu mambo wanayofikiria katika nafsi zao muda wa kuwa hawajafanya wala kuongea (chochote)”(53).

JAMBO LA TATU: KULA NA KUNYWA

Makusudio ya kula na kunywa ni kufikisha chakula au kinywaji tumboni kupitia mdomo au pua. Ama kunusa manukato au harufu yoyote nzuri jambo hilo halifunguzi, kwa sababu hakuna hapo kitu kinachoingia tumboni.

JAMBO LA NNE: KITU CHOCHOTE KINACHOKAA NAFASI YA CHAKULA AU KINYWAJI, NACHO NI AINA MBILI

1) Kuongezewa damu mtu aliyefunga, jambo hili linafunguza.
2) Sindano za vitamin C, kwa sababu imekaa niaba ya chakula.

Ama sindano nyingine haziingii katika hukumu hii hata kama atapata ladha katika koo yake, kwa sababu si chakula wala maji, na wala hazikai niaba ya viwili hivyo.

JAMBO LA TANO: KUFANYA HIJAMA (KUUMIKA/KUPIGA CHUKU)

Hii ni aina ya tiba nzuri ambayo Mtume ﷺ ameisisitiza, tiba hii hufanyika ili kutoa damu chafu mwilini.

Watu hutumia pembe au vikombe na glass maalumu katika kuifanya tiba hii ya hijama. Jambo hili wanachuoni wametafautiana juu ya kufaa kwake kwa mtu aliyefunga, baadhi yao wanaona hadithi iliyokuja kukataza mtu kufanya Hijama hali ya kuwa amefunga imefutwa hukumu yake kwa hadithi nyingine zenye kuruhusu jambo hilo.

Wengine wanaona kwamba mtu anafungua endapo atakuwa amechoka sana na kudhoofika, kwa hiyo iliyo kuwa bora kwa mtu aliyefunga ni kujiepusha na jambo hilo.

Na kwa msimamo wa kwamba jambo hili linabatilisha funga itakuwa haifai kwa mfungaji kumtolea mtu mwingine damu, isipokuwa ikilazimika kufanya hivyo na ikawa hakuna madhara yoyote kwa mfungaji, atafanya hivyo na wakati huo atakuwa amefungua, kwa hiyo atakuja kulipa siku hiyo.

Ama kutokwa na damu za pua, vipele, majipu, kung’oa jino au kujichoma na kitu chenye ncha kali na mfano wake havibatilishi saumu ya mtu, kwa sababu haipatikani katika vitu hivyo athari yoyote kama ilivyokuwa katika tiba ya hijama.

JAMBO LA SITA: KUJITAPISHA:

Kujitapisha ni kukitoa chakula au maji yaliyo matumboni kupitia njia ya mdomo, Mtume ﷺ amesema:

53- Bukhari (5269).

«مَنْ ذَرَعَهُ قَيْءٌ وَهُوَ صَائِمٌ فَلَيْسَ عَلَيْهِ قَضَاءٌ وَإِنِ اسْتَقَاءَ فَلْيَقْضِ»

“Yule ambaye yamemshinda yeye matapishi (hakuweza kujizuia) hali ya kuwa amefunga (akatapika), hakuna juu yake kulipa, na aliyejitapisha na alipe”(54).

Ni sawa amekusudia kwa kitendo kama kukamua tumbo lake n.k, au kwa kunusa kitu chenye kupelekea kutapika, au kwa kutazama kitu chenye kusababisha kutapika.

JAMBO LA SABA: KUTOKA DAMU YA HEDHI AU NIFASI

Mwanamke akiona damu ya Hedhi au Nifasi katika mchana wa Ramadhani funga yake imebatilika, sawa ni mwanzo wa mchana au jioni hata kama ni kitambo kidogo kabla ya kuzama jua.

Ndugu muislamu, mambo hayo saba tuliyoyataja isipokuwa Hedhi na Nifasi hayabatilishi saumu ya mtu isipokuwa kwa masharti matatu:

SHARTI LA KWANZA: MTU AWE ANAJUA HUKUMU YAKE

Kwa kauli ya Allaah:

﴿وَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ فِيمَا أَخْطَأْتُم بِهِۦ وَلَٰكِن مَّا تَعَمَّدَتْ قُلُوبُكُمْ ۚ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا﴾

“Na hapana juu yenu lawama yoyote kwa mlivyokosea. Lakini ipo lawama katika yale ziliyo fanya nyoyo zenu kwa makusudi. Na daima Allaah ni Mwenye kusamehe Mwenye huruma sana”(55).

Ni sawa amefanya kwa kutojua hukumu yake kisheria, mfano amedhani kwamba jambo hilo halibatilishi saumu, au (amefanya) kwa kutojua hali au wakati, kama vile mtu kudhania kwamba jua limezama akala au akadhani kwamba alfajiri bado akaendelea kula daku, mara akasikia watu wanaswali msikitini, katika hali hizo zote haambiwi kwamba funga yake imebatilika.

Lakini akila kwa kudhani kwamba jua limezama kisha ukabainika kwake mchana basi atajizuia mpaka kuzama kwa jua na vivyo hivyo lau kama ameendelea kula kwa dhana ya kwamba bado alfajiri haijachomoza kisha akabainikiwa basi atajizuia mpaka jioni na funga yake ni sahihi wala hakuna kulipa.

SHARTI LA PILI: AWE ANAKUMBUKA

Akifanya moja katika vitenguzi vya saumu kwa kusahau funga yake haibatiliki, kwa hadithi inayosema:

«مَنْ نَسِيَ وَهُوَ صَائِمٌ فَأَكَلَ وَشَرِبَ، فَلْيُتِمَّ صَوْمَهُ، فَإِنَّمَا أَطْعَمَهُ اللَّهُ وَسَقَاهُ»

“Mwenye kusahau akala au akanywa hali ya kuwa amefunga, basi akamilishe saumu yake, hakika Allaah ndiye amemlisha na kumnywesha”(56).

54- Sunan Abi Daud (2382).
55- Surat Al-Ahzaab/5.
56- Bukhari (1933) na Muslim (1155).

Kauli hii ya Mtume ﷺ kwamba akamilishe saumu yake ni ushahidi juu ya usahihi wa saumu yake, na pia kunasibisha kitendo chake cha kula na kunywa kwa Allaah ni ushahidi juu ya kwamba hakuna kosa lolote kwake. Lakini wakati wowote akikumbuka au kukumbushwa atajizuia na atatema kile kilicho mdomoni mwake kwa sababu hana tena udhuru, na mwenye kumuona mtu anakula hali ya kujua kwamba amefunga amkumbushe na huko ni kusaidieni katika wema.

SHARTI LA TATU: AWE AMEFANYE BILA KULAZIMISHWA

Mtu akiyafanya hayo yote yaliyotangulia kwa kulazimishwa, funga yake ni sahihi wala hakuna kulipa, kwa sababu Allaah ameondosha hukumu kwa mtu aliyekufuru kwa kulazimishwa na hali ya kuwa moyo umetulizana katika kumuamini Allaah pekee, ikiwa amesamehewa mtu aliyekufuru basi aliye chini yake katika makosa ni jambo lenye kuwezekana In Shaa Allaah.

Lau mtu akimlazimisha mke wake kufanya naye jimai hali ya kuwa amefunga basi saumu ya mkewe ni sahihi wala hatolipa, lakini naye akiridhia atalipa na pia atahusika na fidia, na kama ni funga ya sunna hakuna ubaya kwake kufungua, pia mwanamke ajue kwamba hatakiwi kufunga sunna isipokuwa kwa idhini ya mume.

Na lau kama limeingia vumbi tumboni kupitia mdomoni au ametawadha akatia maji mdomoni yakapitiliza mpaka tumboni bila kukusudia, funga yake ni sahihi wala hatolipa, kadhaalika haibatiliki funga kwa kutia wanja au dawa machoni au masikioni, hata kama atahisi ladha kwenye koo yake.

Wala haibatiliki funga kwa kuonja chakula endapo hakumeza, wala haibatiliki kwa kunusa harufu ya Udi, lakini asivute moshi wake puani ili asije kufungua, kwa sababu kuna chembechembe zinapanda na moshi huo huenda zikapenya na kuingia tumboni.

Vilevile haibatiliki saumu kwa kupiga mswaki, bali ni sunna kupiga mswaki wakati wa asubuhi mpaka jioni kwa mfungaji na asiye kuwa mfungaji, lakini kwa mfungaji ni vizuri asitumie dawa ya meno.

Pia Inafaa kwa mtu aliyefunga kutumia kitu kwa ajili ya kupoza joto mwilini mwake kama vile kujimwagia maji baridi kichwani mwake n.k.

Allaah aturuzuku Ikhlaas katika kauli na amali.

DARASA YA NNE
MAMBO ALIYORUHUSIWA MFUNGAJI NA YALE ALIYOKATAZWA

1. KUCHELEWESHA KUOGA JANABA AU HEDHI MPAKA ASUBUHI

Amesimulia Aisha na Ummu Salama (Allaah awaridhie) kwamba Mtumeﷺ alikuwa:

«يُدْرِكُهُ الفَجْرُ وَهُوَ جُنُبٌ مِنْ أَهْلِهِ، ثُمَّ يَغْتَسِلُ، وَيَصُومُ»

“Inamdiriki yeye alfajiri na hali ya kuwa ana janaba kutokana na wakeze, kisha anaoga na anafunga”[57].

Baadhi ya watu hudhani kwamba mtu ukiamka na janaba asubuhi ya Ramadhani saumu yake haisihi, hapana, hadithi hii inapingana na dhana hiyo.

2. KUOGA AU KUJIMWAGIA KICHWANI KWA AJILI YA JOTO KALI

Amesimulia mmoja kati ya Maswahaba wa Mtumeﷺ kwamba:

«لقد رأيتُ رسولَ الله -صلَّى الله عليه وسلم- بالعَرْجِ يصُبُّ على رأسِه الماءَ وهو صَائِمٌ مِن العَطَشِ، أَوْ مِن الحَرِّ»

“Hakika nilimuona Mtumeﷺ sehemu (inayoitwa) ‘Arji anajimwagia maji kichwani mwake hali ya kuwa amefunga kutokana na Kiu au Joto kali”[58].

Amesema Imam Ibn Qudama (Allaah amrehemu):

"وَلَا بَأْسَ أَنْ يَغْتَسِلَ الصَّائِمُ"

“Wala hapana vibaya kuoga (mchana) kwa mfungaji”[59].

Na amesema Sharaful Haqqi (Allaah amrehemu) kuhusu hadithi hii:

"فِيهِ دَلِيلٌ عَلَى أَنَّهُ يَجُوزُ لِلصَّائِمِ أَنْ يَكْسِرَ الْحَرَّ بِصَبِّ الْمَاءِ عَلَى بَعْضِ بَدَنِهِ أَوْ كُلِّهِ"

“Kuna katika hadithi hii dalili juu ya kwamba inafaa kwa mfungaji kukata joto kwa kujimwagia maji katika baadhi ya (sehemu ya) mwili wake au (kuoga) mwili wake wote”[60].

3. KUMKUMBATIA AU KUM’BUSU MKEO MCHANA WA RAMADHANI

Amesimulia Aisha (Allaah amridhie), alikuwa Mtumeﷺ:

«يُقَبِّلُ وَيُبَاشِرُ وَهُوَ صَائِمٌ، وَكَانَ أَمْلَكَكُمْ لِإِرْبِهِ»

57- Bukhari (1926).
58- Sunan Abi Daud (2365).
59- Al-Mughni (Jz. 3, Uk. 124).
60- ‘Aunul Ma’buud (Jz. 6, uk. 352).

“Anabusu na kukumbatia hali ya kuwa amefunga, na alikuwa anamiliki zaidi matamanio yake”[61].

Amesema Ibn Qudama (Allaah amrehemu):

"فَإِنَّ الْمُقَبِّلَ إِذَا كَانَ ذَا شَهْوَةٍ مُفْرِطَةٍ، بِحَيْثُ يَغْلِبُ عَلَى ظَنِّهِ أَنَّهُ إِذَا قَبَّلَ أَنْزَلَ، لَمْ تَحِلَّ لَهُ الْقُبْلَةُ؛ لِأَنَّهَا مُفْسِدَةٌ لِصَوْمِهِ"

“Akiwa mwenye kubusu ni mtu mwenye matamanio yaliyozidi, kiasi inashinda katika dhana yake kwamba akibusu atateremsha manii, basi haitafaa kwake kubusu, kwa sababu jambo hilo ni lenye kupelekea kuharibu funga yake”[(62)].

Pia amesema Imam Nnawawi (Allaah amrehemu):

"ذَكَرْنَا أَنَّ مَذْهَبَنَا كَرَاهَتُهَا لِمَنْ حَرَّكَتْ شَهْوَتَهُ وَلَا تُكْرَهُ لِغَيْرِهِ وَالْأَوْلَى تَرْكُهَا"

“Tumetangulia kutaja madhehebu yetu kwamba jambo hilo ni karaha (haramu) kwa mtu ambaye (huko kubusu) kutachochea matamanio yake, na wala si haramu kwa mtu mwingine asiyekuwa huyo. Na iliyo bora ni kuacha”[(63)].

AMA MAMBO ALIYOKATAZWA:

4. ASIZUNGUMZE MANENO YA MCHEZO NA UPUUZI

«إِنَّ الصِّيَامَ لَيْسَ مِنَ الْأَكْلِ وَالشُّرْبِ فَقَطْ، إِنَّمَا الصِّيَامُ مِنَ اللَّغْوِ وَالرَّفَثِ»

“Funga si kuacha kula na kunywa tu, hakika funga ni kujiepusha na pumbao na maneno machafu”[(64)].

5. KUSAMEHE NA KUACHA KUPIGA MAKELELE

«وَإِذَا كَانَ يَوْمُ صَوْمِ أَحَدِكُمْ فَلاَ يَرْفُثْ وَلاَ يَصْخَبْ، فَإِنْ سَابَّهُ أَحَدٌ أَوْ قَاتَلَهُ فَلْيَقُلْ إِنِّي امْرُؤٌ صَائِمٌ»

“Itakapokuwa siku ya funga ya mmoja wenu asiseme maneno machafu, wala asipige kelele, na mtu yeyote akimtukana au kutaka kupigana nae basi aseme: mimi ni mtu niliyefunga”[(65)].

6. ASIBALIGHISHE MAJI PUANI KATIKA WAKATI WA KUCHUKUA UDHU

Sunna ni kutia maji puani na kuyavuta wakati wa kutawadha (kubalighisha), kisha kuyapenga kwa mkono wa kushoto, lakini hilo halifai kwa mfungaji, kadhaalika kuna baadhi yao wanapotawadha hutia vidole puani badala ya maji na wengine hupenga kwa kutumia mkono wa kulia, haya yote ni makosa.

«وَبالِغْ فِي الاستِنشاقِ إلا أَنْ تَكُوْنَ صَائِماً»

“Na balighisha wakati wa kupandisha maji puani isipokuwa uwe umefunga”[(66)].

61- Bukhari (1927) na Muslim (1106).
62- Al-Mughni (Jz. 4, Uk. 361).
63- Al-Majmuu’ sharhil Muhaddhab (Jz. 6 Uk. 355)
64- Sahihi Bin Hibbaan (3479).
65- Bukhari (1904) na Muslim (1151).
66- Sunan Abi Daud (142).

DARSA YA TANO
FADHILA ZA KISIMAMO CHA RAMADHANI NA MASIKU KUMI YA MWISHO

SWALA YA TARAWEIH NI SABABU YA KUFUTIWA MADHAMBI

«مَنْ قَامَ رَمَضَانَ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا، غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ»

“Mwenye kusimama (kuswali) katika mwezi wa Ramadhani kwa Imani na kutarajia malipo, atasamehewa madhambi yake yaliyopita”[67].

NAMNA YA KISIMAMO (SWALA) YA MTUME ﷺ USIKU:

Amesema Aisha (Allaah amridhie):

"مَا كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَزِيدُ فِي رَمَضَانَ، وَلَا فِي غَيْرِهِ، عَلَى إِحْدَى عَشْرَةَ رَكْعَةً، يُصَلِّي أَرْبَعًا، فَلَا تَسْأَلْ عَنْ حُسْنِهِنَّ وَطُولِهِنَّ، ثُمَّ يُصَلِّي أَرْبَعًا، فَلَا تَسْأَلْ عَنْ حُسْنِهِنَّ وَطُولِهِنَّ، ثُمَّ يُصَلِّي ثَلَاثًا"

“Hakuwa Mtume ﷺ akizidisha katika mwezi wa ramadhani wala miezi mingine zaidi ya rakaa kumi na moja. Alikuwa anaswali rakaa nne, basi usiulize kuhusu uzuri wake na urefu wake, kisha anaswali (tena) rakaa nne, basi usiulize kuhusu uzuri wake na urefu wake, kisha anaswali rakaa tatu”[68].

Kuna khilafu baina ya wanachuoni kuhusu kuswali Taraweih zaidi ya rakaa kumi na moja, kuna wanaosema sunnah ni kuswali rakaa hizo kumi na moja (rakaa nane za taraweih na rakaa tatu za witri) kwa hadithi iliyotangulia, na wengine wanaona kwamba Mtume ﷺ aliswali rakaa hizo kumi na moja lakini hakuweka ukomo, kwa hiyo mtu anaruhusiwa kuongeza kama iivyopokewa kwa baadhi ya Salaf, na wengine wamefafanua kwamba ukirefusha kisomo utaswali rakaa kumi na moja lakini kama utafupisha basi swali rakaa nyingi zaidi ya kumi na moja, kama walivyosema hilo baadhi ya Salaf.

Pia Mtume ﷺ amesema huku akitoa mwongozo wa namna ya kuswali swala za usiku, akasema:

«مَثْنَى مَثْنَى، فَإِذَا خَشِيَ الصُّبْحَ صَلَّى وَاحِدَةً، فَأَوْتَرَتْ لَهُ مَا صَلَّى»

“(Swala ya usiku) ni rakaa mbili mbili, akihofia kudirikiwa na asubuhi ataswali rakaa moja, itakuwa ndio witri yake kwa kile alichoswali”[69].

67- Bukhari (37) na Muslim (759).
68- Sunan Abi Daud (1341).
69- Bukhari (472).

SWALA YA WITRI:

Witri ni swala ambayo huswaliwa mwisho wa swala za usiku kwa kauli ya Mtume ﷺ na pia unaweza kuswali kabla ya kulala:

«اجْعَلُوا آخِرَ صَلَاتِكُمْ بِاللَّيْلِ وِتْرًا»

“Ijaalieni mwisho wa swala yenu wakati wa usiku kuwa ni witri”(70).

INAJUZU KUSWALI WITRI RAKAA MOJA:

«الْوِتْرُ حَقٌّ، فَمَنْ أَحَبَّ أَنْ يُوتِرَ بِخَمْسٍ رَكَعَاتٍ فَلْيَفْعَلْ، وَمَنْ أَحَبَّ أَنْ يُوتِرَ بِثَلَاثٍ فَلْيَفْعَلْ، وَمَنْ أَحَبَّ أَنْ يُوتِرَ بِوَاحِدَةٍ فَلْيَفْعَلْ»

“Witri ni haki, anaependa kuswali witri rakaa tano na afanye, anaependa kuswali witri rakaa tatu na afanye na anaependa kuswali rakaa moja na afanye”(71).

Amesema Zainu Ddiin Al-‘Iraaqi (Allaah amrehemu):

"وَمَذْهَبُ مَالِكٍ وَالشَّافِعِيِّ وَأَحْمَدَ وَالْجُمْهُورِ جَوَازُ الْوِتْرِ بِرَكْعَةٍ فَرْدَةٍ"

“Na madhehebu ya Malik, Shaafi’, Ahmad na wengi katika maulamaa (Jumhuri) ni kufaa kuswali witri rakaa moja”(72).

INAJUZU KUSWALI WITRI RAKAA TATU:

Anasema Ubayyu Ibn Ka’b (Allaah amridhie):

"كَانَ يُوتِرُ بِثَلَاثِ رَكَعَاتٍ، كَانَ يَقْرَأُ فِي الْأُولَى بِسَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى، وَفِي الثَّانِيَةِ بِقُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ، وَفِي الثَّالِثَةِ بِقُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ"

“Mtume ﷺ alikuwa anaswali witri rakaa tatu, katika rakaa ya kwanza alikuwa anasoma Sabbihisma (Suratul A’alaa), na katika rakaa ya pili Suratul Kafiruun na katika rakaa ya tatu Suratul Ikhlaas”(73).

WITRI YA RAKAA TATU NA UFAFANUZI WAKE

Swala ya witri ni aina nyingi, rakaa tatu, tano, saba, tisa na kumi na moja, lakini hapa nimeona nitaje aina mbili pekee (rakaa moja na rakaa tatu) na ufafanuzi wake.

Amesema sheikh Ibn Uthaymin (Allaah amrehemu):

"فَإِذَا أَوْتَرَ الإِنْسَانُ بِثَلَاثِ رَكَعَاتٍ فَإِنَّهُ مُخَيَّرٌ بَيْنَ أَنْ يُصَلِّيَهَا بِتَسْلِيمَتَيْنِ يَعْنِي يُصَلِّي رَكْعَتَيْنِ ثُمَّ يُسَلِّمُ، ثُمَّ يُصَلِّي الثَّالِثَةَ وَحْدَهَا، أَوْ أَنْ يَسْرُدَهَا جَمِيعًا بِتَشَهُّدٍ وَاحِدٍ عِنْدَ السَّلَامِ".

“Mtu atakaposwali witri ya rakaa tatu amepewa hiyari (atachagua) baina ya kuswali kwa salamu mbili, maana yake ataswali rakaa mbili kisha atatoa salamu,

70- Sahihi Muslim (151).
71- Bukhari (472).
72- Sunan Nnasaai (1712).
73- Sunan Nnasaai (1699).

halafu ataswali rakaa (moja) ya tatu, au ataunganisha zote (rakaa tatu) kwa kusoma Tashah-hud moja tu wakati wa kutoa salamu”[74].

KISOMO KATIKA SWALA YA WITRI

Amesema Sheikh Ibn Uthaimin (Allaah amrehemu):

وَأَمَّا الْقِرَاءَةُ: فَيَقْرَأُ مَا تَيَسَّرَ لَهُ سَوَاءٌ أَوْتَرَ بِوَاحِدَةٍ، أَوْ ثَلَاثٍ، أَوْ خَمْسٍ أَوْ تِسْعٍ أَوْ إِحْدَى عَشْرَةٍ، إِلَّا إِذَا أَوْتَرَ بِثَلَاثٍ، فَالْأَفْضَلُ أَنْ يَقْرَأَ فِي الْأُوْلَى (سَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى). وَفِي الرَّكْعَةِ الثَّانِيَةِ: (قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ). وَفِي الرَّكْعَةِ الثَّالِثَةِ: (قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ)

“Ama kisomo: atasoma anachokijua katika Qur’an, ni sawa aliswali witri rakaa moja, tatu, tano, tisa au kumi na moja, isipokuwa akiswali witri ya rakaa tatu iliyo bora ni kuwa asome katika rakaa ya kwanza (Sabbihisma), rakaa katika ya pili Surat (Al-Kafiruun) na katika rakaa ya tatu (asome): Suratul Ikhlaas”[75].

QUNUUT YA WITRI[76]

Mtu anapofika rakaa ya mwisho ya swala ya witri ni sunna kwake kusoma Qunuut, ima kabla au baada ya kurukuu, katika dua hiyo atanyanyua mikono na ataitikia Aamiin yule aliye nyuma yake (maamuma), isipokuwa baadhi ya matamko hataitikia Aamiin kama tutakavyobainisha In Shaa Allaah. Na Mtume ﷺ ndiye aliyemfundisha mjukuu wake Hassa na Hussein (Allaah awaridhie) dua hii ya Qunuut.

«اللَّهُمَّ اهْدِنِي فِيمَنْ هَدَيْتَ، وَعَافِنِي فِيمَنْ عَافَيْتَ، وَتَوَلَّنِيفِيمَنْ تَوَلَّيْتَ، وَبَارِكْ لِي فِيمَا أَعْطَيْتَ، وَقِنِي شَرَّ مَا قَضَيْتَ، إِنَّكَ تَقْضِي وَلَا يُقْضَى عَلَيْكَ، وَإِنَّهُ لَا يَذِلُّ مَنْ وَالَيْتَ، وَلَا يَعِزُّ مَنْ عَادَيْتَ، تَبَارَكْتَ رَبَّنَا وَتَعَالَيْتَ»

“Ewe Allaah niongoze niwe miongoni mwa uliye muongoza. Na unipe afya niwe miongoni mwa aliyempa afya. Na ninusuru mimi niwe miongoni mwa uliyemnusuru. Na nibariki kwenye kile ulichonipatia. Na nikinge na shari ya lile ambalo umekadiria. Hakika wewe unahukumu wala uhukumiwi. Hakika hapati udhalili yule ambaye umemtawalia. Wala hawezi kupata nguvu yule uliyemfanya adui. Umetukuka Ewe Mola wetu Mlezi, na umekuwa juu”[77].

HUKUMU YA KUZIDISHA KATIKA QUNUUT

Amesema sheikh Ibn Uthaymin (Allaah amrehemu):

"لَوْ زَادَ إِنْسَانٌ عَلَى ذَلِكَ فَلَا بَأْسَ، لِأَنَّ المَقَامَ مَقَامُ دُعَاءٍ"

“Lau mtu atazidisha juu ya dua hiyo basi hapana vibaya, kwa sababu hapo ni mahala pa kuomba dua”[78].

74- Majmuu’ Fataawa warasaail (Jz. 14, Uk. 110).
75- Majmuu’ Fataawa warasaail (Jz. 14, Uk. 71).
76- Kuhusu ufafanuzi wa Qunuut nitaituma Makala maalumu hivi karibuni In Shaa Allaah.
77- Abu Daud (1425).
78- As Sharhul Mummti’ (Jz. 4, Uk. 38).

JE UTAITIKIA AAMIIN PINDI IMAMU AKIMSIFU ALLAAH KATIKA QUNUUT?

Amesema Imam Nnawawi (Allaah amrehemu):

"وَأَمَّا الثَّنَاءُ وَهُوَ قَوْلُهُ فَإِنَّكَ تَقْضِي وَلَا يُقْضَى عَلَيْكَ إِلَى آخِرِهِ فَيُشَارِكُهُ فِي قَوْلِهِ أَوْ يَسْكُتُ وَالْمُشَارَكَةُ أَوْلَى لِأَنَّهُ ثَنَاءٌ وَذِكْرٌ لَا يَلِيقُ فِيهِ التَّأْمِينُ".

“Ama kumsifia (Allaah) nayo ni kauli yake (Fainnaka taqdhwii wala yuqdhwaa alaika…) mpaka mwisho wa Qunuut, (maamuma) atashirikiana na (imamu) wake katika kauli yake hiyo au atanyamaza, na kushirikiana nae ni bora, kwa sababu (maneno) hayo ni dhikri na ni sifa na dhikri haifai kuitikia Aamiin”. [Sharhul muhaddhab (Jz. 3, Uk. 502)].

HUKUMU YA KUMSWALIA MTUME ﷺ MWISHO WA QUNUUT

Amesema Mtume ﷺ:

«إِنَّ الدُّعَاءَ مَوْقُوفٌ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالأَرْضِ لَا يَصْعَدُ مِنْهُ شَيْءٌ، حَتَّى تُصَلِّيَ عَلَى نَبِيِّكَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ»

“Dua ni yenye kusangazwa baina ya mbingu na ardhi, hakuna chochote kinachopanda (mbinguni) katika dua mpaka umswalie Mtume wako ﷺ”[79].

Amesema sheikh Ibn Uthaymin (Allaah amrehemu):

"يَخْتِمُ الدُّعَاءَ بِالصَّلَاةِ عَلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ؛ لِأَنَّ ذَلِكَ مِنْ أَسْبَابِ الْإِجَابَةِ"

“Atakhitimisha dua (yake) kwa kumswalia Mtume ﷺ, kwa sababu kufanya hivyo ni miongoni mwa sababu za kujibiwa dua”[80].

KUPANGUSA MIKONO USONI BAADA YA QUNUUT:

Amesema Imam Nnawawi (Allaah amrehemu):

"لَا يَمْسَحُ وَهَذَا هُوَ الصَّحِيحُ، صَحَّحَهُ الْبَيْهَقِيُّ وَالرَّافِعِيُّ وَآخَرُونَ مِنْ الْمُحَقِّقِينَ قَالَ الْبَيْهَقِيُّ لَسْتُ أَحْفَظُ فِي مَسْحِ الْوَجْهِ هُنَا عَنْ أَحَدٍ مِنْ السَّلَفِ شَيْئًا... فَالْأَوْلَى أَنْ لَا يَفْعَلَهُ وَيُقْتَصَرَ عَلَى مَا نَقَلَهُ السَّلَفُ عَنْهُمْ مِنْ رَفْعِ الْيَدَيْنِ دُونَ مَسْحِهِمَا بِالْوَجْهِ فِي الصَّلَاةِ"

“Hapangusi (uso wake), na hii ndio kauli sahihi ambayo ameisahihisha Al-Baihaqi, Ar-Raafii’ na wengine katika wanachuoni wenye kuhakiki (mambo), amesema Al-Baihaqi: Sijahifadhi kauli yoyote kutoka kwa Salaf (wema waliotangulia) kuhusiana na kupangusa uso sehemu hii…… iliyo bora ni mtu kutofanya hivyo na hutosheleza kile walichonukuu Salaf kutoka kwao (Maswahaba), ambacho ni kunynayua mikono tu bila kuipangusa usoni ndani ya swala”[81].

79- Sunan Tirmidh (486).

80- As Sharhul Mummti’ (Jz. 4, Uk. 38).

81- [Majmuu’ sharhil muhaddhab], (Jz. 3, Uk. 501).

Jawabu la Al-Lajna Ddaaima kuhusiana na kupangusa uso baada ya kuomba dua:

"وَأَمَّا مَسْحُ الوَجْهِ بِالْكَفَّيْنِ عَقِبَ الدُّعَاءِ فَقَدْ وَرَدَ فِيْهِ حَدِيْثٌ ضَعِيْفٌ... وَلَمَّا كَانَ الدُّعَاءُ عِبَادَةً مَشْرُوْعَةً، وَلَمْ يَثْبُتْ فِيْ مَسْحِ الوَجْهِ بِالْكَفَّيْنِ سُنَّةٌ قَوْلِيَّةٌ أَوْ عَمَلِيَّةٌ، بَلْ رُوِيَ ذَلِكَ مِنْ طُرُقٍ ضَعِيْفَةٍ - فَالْأَوْلَى تَرْكُهُ، عَمَلًا بِالْأَحَادِيْثِ الصَّحِيْحَةِ الَّتِيْ لَمْ يُذْكَرْ فِيْهَا الْمَسْحُ"

“Hakika imekuja hadithi dhaifu kuhusu kupangusa uso kwa viganja viwili baada ya kumaliza kuomba dua, na wakati ilipokuwa dua ni ibada yenye kuwekewa sheria na haijathibiti katika kupangusa uso sunna yoyote ya matendo wala maneno, bali limepokewa hilo kwa njia ambazo ni dhaifu, basi iliyo bora ni kuliacha kwa ajili ya kufanyia kazi hadithi ambazo ni sahihi, ambazo hakujatajwa ndani yake kupangusa”[82].

ADHKAAR BAADA YA KUMALIZA SWALA YA WITRI

Imekuja katika hadithi ya Ubayyu Bin Ka’b (Allaah amridhie):

"فَإِذَا فَرَغَ، قَالَ: عِنْدَ فَرَاغِهِ: «سُبْحَانَ الْمَلِكِ الْقُدُّوسِ». ثَلَاثَ مَرَّاتٍ يُطِيلُ فِي آخِرِهِنَّ"

“Anapomaliza anasema: (Subhaanal Malikil Qudduus) mara tatu, na mara ya mwisho ananyanyua sauti”[83].

Na imekuja ziada katika riwaya nyingine:

"رَبُّ المَلَائِكَةِ وَالرُّوْحِ"

“Mola Mlezi wa Malaika na Jibril”[84].

82- [Fataawa Llajna Ddaaima], (Jz. 4, Uk. 445).

83- Sunan Nnasaai (1669). Maana yake: **[Utakasifu ni wa mfalme asiye na mapungufu].**

84- Sunan ddaraqutni (Jz. 2, Uk. 355) 1660

DARASA YA SITA
FADHILA ZA KUKAA ITIKAFU NA KUITAFUTA LAYLATIL QADRI

MAANA YA ITIKAFU:

Maana ya Itikafu katika lugha ya kiarabu ni: kulazimiana na kitu (iwe kheri au shari) na kuifunga nafsi juu yake.

Ama kisheria ni: Mtu kulazimiana na msikiti kwa ajili ya kujikurubisha kwa Allaah kwa sifa maalumu.

Nguzo zake ni: Nia, kukaa msikitini, kupatikana mwenye kukaa Itikafu (muislamu, mwenye akili) na mwanamke apate idhini ya mume, na kuwepo mahala pa kukaa Itikafu (msikiti unaoswaliwa jamaa (na iliyo bora iwe katika msikiti unaoswali Ijumaa). Amesema Ibn Qudama:

وَإِنَّمَا اشْتُرِطَ ذَلِكَ؛ لِأَنَّ الْجَمَاعَةَ وَاجِبَةٌ، وَاعْتِكَافُ الرَّجُلِ فِي مَسْجِدٍ لَا تُقَامُ فِيهِ الْجَمَاعَةُ يُفْضِي إِلَى أَحَدِ أَمْرَيْنِ: إمَّا تَرْكُ الْجَمَاعَةِ الْوَاجِبَةِ، وَإِمَّا خُرُوجُهُ إلَيْهَا، فَيَتَكَرَّرُ ذَلِكَ مِنْهُ كَثِيرًا مَعَ إمْكَانِ التَّحَرُّزِ مِنْهُ، وَذَلِكَ مُنَافٍ لِلِاعْتِكَافِ،

“**Limeshurutishwa jambo hilo, kwa sababu kuswali jamaa ni wajibu (kwa mwanaume), na mtu kukaa Itikafu katika msikiti ambao hauswaliwi jamaa kunapelekea kwenye moja ya mambo mawili: Kuacha swala ya jamaa ambayo ni wajibu, au kutoka kuifuata jamaa, mwisho wake litajikariri jambo hilo kwake pamoja na kuwezekana kuliepuka, na jambo hilo (kutoka mara kwa mara) kunapingana na itikafu”[85].**

Pia wamekubaliana maulamaa wote kwamba Itikafu itafisidika kwa kufanya jimai kwa makusudi.

KUWEKEWA KWAKE SHERIA

Amesema Allaah Ta’alaa:

﴿ وَلَا تُبَٰشِرُوهُنَّ وَأَنتُمْ عَٰكِفُونَ فِي ٱلْمَسَٰجِدِ ﴾

“Wala amsichanganyike nao (kwa jimai) na hali mnakaa Itikafu misikitini”[86].

Na imepokewa hadithi kutoka kwa Aisha (Allaah amridhie):

«أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، كَانَ يَعْتَكِفُ العَشْرَ الأَوَاخِرَ مِنْ رَمَضَانَ حَتَّى تَوَفَّاهُ اللَّهُ، ثُمَّ اعْتَكَفَ أَزْوَاجُهُ مِنْ بَعْدِهِ»

“Kwamba Mtume ﷺ, alikuwa anakaa Itikafu masiku kumi ya mwisho ya ramadhani, mpaka Allaah alipomfisha, kisha wakakaa Itikafu wakeze baada yake”[87].

85- Al-Mughni (Jz. 3, Uk. 189).
86- Surat Al-Baqara/187.
87- Bukhari (2026) na Muslim (1172).

HUKUMU YA KUKAA ITIKAFU

Amesema Imam Nnawawi (Allaah amrehemu):

"فَالِاعْتِكَافُ سُنَّةٌ بِالْإِجْمَاعِ وَلَا يَجِبُ إِلَّا بِالنَّذْرِ بِالْإِجْمَاعِ وَيُسْتَحَبُّ الْإِكْثَارُ مِنْهُ وَيُسْتَحَبُّ وَيَتَأَكَّدُ اسْتِحْبَابُهُ فِي الْعَشْرِ الْأَوَاخِرِ مِنْ شَهْرِ رَمَضَانَ"

“Itikafu ni sunna kwa makubaliano (ya maulamaa) wala si wajibu isipokuwa kwa nadhiri, na inahimizwa na kukokotezwa zaidi sunna yake katika siku kumi za mwisho za mwezi wa ramadhani”[88].

JE ATAKAA ITIKAFU PASI NA KUFUNGA

Kuna khilafu kuhusu sharti la saumu kwa mwenye kukaa Itikafu, kuna wanaoona ni sharti awe amefunga, na wengine wanaona hilo si sharti.

Lakini amesema Ibnul Qayyim (Allaah amrehemu):

"وَلَمْ يَذْكُرِ اللَّهُ سُبْحَانَهُ الِاعْتِكَافَ إِلَّا مَعَ الصَّوْمِ، وَلَا فَعَلَهُ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِلَّا مَعَ الصَّوْمِ"

“Allaah hakuitaja Itikafu isipokuwa (ameitaja) pamoja na saumu, wala Mtume ﷺ hakukaa Itikafu isipokuwa pamoja na saumu (akiwa amefunga)”[89].

Na pia amesema Al-Qadhi ‘Iyadh Bin Musa (Allaah amrehemu):

"وَهَذَا الْقَوْلُ هُوَ الْقَوِيُّ إِنْ شَاءَ اللَّهُ، وَهُوَ أَنَّ الصِّيَامَ شَرْطٌ فِي الِاعْتِكَافِ"

“Na kauli hii ndio yenye nguvu In Shaa Allaah, nayo ni kwamba saumu ni sharti katika (kukaa) Itikafu”[90].

MUDA WA KUINGIA MAHALA PA ITIKAFU NA MUDA WA KUTOKA KWAKE

Amesema Aisha (Allaah amridhie):

«كَانَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، إِذَا أَرَادَ أَنْ يَعْتَكِفَ صَلَّى الْفَجْرَ، ثُمَّ دَخَلَ مُعْتَكَفَهُ»

“Mtume ﷺ alikuwa anapotaka kukaa Itikafu anaswali (swala ya) alfajri, kisha anaingia mahala pake pa Itikafu”[91].

Amesema sheikh Ibn Uthaymin (Allaah amrehemu):

"جُمْهُوْرُ أَهْلِ الْعِلْمِ عَلَى أَنَّ ابْتِدَاءَ الِاعْتِكَافِ مِنْ لَيْلَةِ إِحْدَى وَعِشْرِيْنَ لَا مِنْ فَجْرِ إِحْدَى وَعِشْرِيْنَ... لِأَنَّ الْعَشْرَ الْأَوَاخِرَ تَبْتَدِيءُ مِنْ غُرُوْبِ الشَّمْسِ يَوْمَ عِشْرِيْنَ. يَخْرُجُ الْمُعْتَكِفُ مِنِ اعْتِكَافِهِ إِذَا انْتَهَى رَمَضَانُ، وَيَنْتَهِيْ رَمَضَانُ بِغُرُوْبِ الشَّمْسِ لَيْلَةَ الْعِيْدِ"

88- Al-Majmuu’ (Jz. 6, Uk. 475).
89- Zaadul Ma’ad (Jz, 2, Uk. 87).
90- Nasbu Rraayah (Jz. 2, Uk. 489).
91- Bukhari (2041) na Muslim (1173).

“Wengi katika wanachuoni wanaona kwamba Itikafu itaanza usiku wa kuamkia (tarehe) ishirini na moja na si alfajri ya siku hiyo (tarehe 21)… kwa sababu masiku kumi ya mwisho yanaanzia tangu kuzama jua siku ya (tarehe) ishirini. Na atatoka katika mahala pake pa Itikafu itakapomalizika ramadhani, na ramadhani inamalizika kwa kuzama jua usiku wa (kuamkia) Eid”.

MAMBO YANAYOMHUSU MWENYE KUKAA ITIKAFU

Makusudio ya kukaa Itikafu ni kuizuia nafsi juu ya kufanya mambo ya kujikurubisha kwa Allaah, na asili ni kwamba asifanye isipokuwa mambo yanayohusika na msikiti, ambayo ni swala, dhikri na kusoma Qur’an.

MAMBO YALIYO MUBAHA KWA MWENYE KUKAA ITIKAFU

- Inafaa kwake kutoka kwa ajili ya kukidhi haja, kuchukua chakula na kinywaji, ikiwa hakuna mtu wa kumletea.
- Inafaa kwake kutoka kwa ajili ya kuoga, kutawadha n.k.
- Inafaa kake kuosha nywele zake na kuzichana.

Amesema Imam Al-Khatwab (Allaah amrehemu) wakati akielezea hadithi ya Aisha (Allaah amridhie) kwamba Mtume ﷺ wakati yupo katika Itikafu alikuwa anakitoa kichwa chake na Aisha anamchana nywele zake akiwa nyumbani kwake:

"وَفِيْ مَعْنَاهُ حَلْقُ الرَّأْسِ وَتَقْلِيْمُ الأَظْفَارِ وَتَنْظِيْفُ البَدَنِ مِنَ الشَّعَثِ وَالدَّرَنِ"

“Na katika maana yake ni (kufaa) kunyoa nywele, kukata kucha na kuusafisha mwili kutokana na vumbi na uchafu”[92].

- Inafaa kujitengenezea hema ndani ya msikiti.
- Inafaa kwake kujipaka mafuta na kujitia manukato.
- Inafaa kukaa Itikafu kwa mwanamke mwenye Istihadha.
- Inafaa kwake kutembelewa na watu kama vile mkewe n.k.
- Inafaa kwake kumsindikiza mgeni wake mpaka mlango wa msikiti.

MAMBO YASIYOFAA KWA MWENYE KUFANYA ITIKAFU:

- Haifai kwake kufanya jimai na mke wake kwa sababu jambo hilo linabatilisha Itikafu yake, tena baadhi ya wanachuoni wanasema itaingia katika katazo pia kumkumbatia mkewe, kugisana nae hata kwa kupeana nae mkono na kulala nae pamoja, kwa sababu mambo hayo yanachochea jiami.
- Asitoke kwa ajili ya kwenda kumtazama mgonjwa.
- Asitoke kwa ajili ya kwenda kusindikiza jeneza.

92- Ma’alimu Ssunan (Jz. 2, Uk. 140).

FADHILA ZA KUITAFUTA LAYLATUL QADRI (USIKU WENYE CHEO)

Laylatul Qadri ni usiku wenye cheo na daraja kubwa mbele ya Allaah Ta'alaa, kwa sababu ni usiku ambao ndani yake imeteremshwa Qur'an, kitabu ambacho ndani yake kuna mwongozo na nuru kwa watu, kwa hiyo hii ni fursa muhimu kwa muislamu kujitahidi kumuomba Mola wake haja zake mbalimbali, kubwa zaidi ni kumuomba yeye Allaah msamaha wa madhambi yake.

Usiku huu unapatikana katika masiku kumi ya mwisho wa mwezi wa ramadhani tu, hasa hasa masiku ya witri, hali ya kuwa ni fadhila ya Allaah kwa umma huu tu.

Hakika huu ni usiku wenye baraka nyingi, huteremka ndani yake Malaika pamoja na Jibril (alaihimus salaam) na pia ni usiku ambao hupangwa matendo ya waja na kupambanuliwa kwa muda wa mwaka mzima, usiku huo ni salama mpaka asubuhi yake.

Mtume ﷺ alikuwa anajitahidi sana kufanya ibada katika masiku kumi haya pia kuwahimiza wakeze na watu wa nyumbani kwake mpaka, akafikia kusema hali ya kutuhimiza:

«تَحَرَّوْا لَيْلَةَ القَدْرِ فِي الوِتْرِ، مِنَ العَشْرِ الأَوَاخِرِ مِنْ رَمَضَانَ»

"Itafuteni Laylatul Qadri katika (masiku ya) witri katika masiku kumi ya mwisho ya ramadhani"[93]".

Na Aisha (Allaah amridhie) alipoulizwa kuhusu dua ya kusoma endapo atajua kuwa huo ndio usiku wa Laylatul Qadri, Mtume ﷺ akasema:

«قُولِي: اللَّهُمَّ إِنَّكَ عَفُوٌّ تُحِبُّ الْعَفْوَ فَاعْفُ عَنِّي»

"Sema: Ewe Allaah, hakika wewe ni mwingi wa msamaha unapenda kusamehe, basi nisamehe mimi"[94].

Kwa hiyo mtu anatakiwa asome kwa wingi dua hii katika masiku haya hasa wakati wa usiku, lakini haijathibiti ziada ya neno (Kariim) kama wanavyo fanya baadhi ya watu:

اللَّهُمَّ إِنَّكَ عَفُوٌّ كَرِيمٌ

Pia kuna baadhi ya watu wameifanya dua hii kuwa ni uradi wao wa mwezi wa ramadhani, wanaisoma kila baada ya swala ya faradhi kuanzia mwanzo wa ramadhani mpaka mwisho wake, jambo hili halijathibiti.

Ndugu muislamu Allaah Ta'alaa ameuficha usiku huo ili watu wajitahidi kufanya ibada katika kuutafuta kwake, kwa hiyo watu wautafute kwa kukaa Itikafu, kusimama kwa Imani na kutaraji malipo, kuomba dua, kuwahamsha watu wa nyumbani kwa ajili ya ibada, pia umefichwa usiku huo ili iwe ni mtihani kwao ili apate kujulikana ni nani miongoni mwao ana pupa zaidi ya kupata rehma za Allaah Subhaanah.

93- Bukhari (2017) na Muslim (1169).
94- Sunan Tirmidh (3513).

Ndugu muislamu Laylatul Qadri haitokei katika usiku mmoja tu kila mwaka, huenda mwaka huu ikapatikana katika usiku wa tarehe 27 na mwakani ikatokea katika usiku wa 21 n.k, ili watu watoe juhudi katika masiku kumi yote ya mwisho wa ramadhani.

Wala haikuja Laylatul Qadri ili watu waombe mambo ya dunia yao, kama zile simulizi za zamani za uwongo kwamba Laylatul Qadri ni mwanga mkubwa unaotoka mbinguni na kuenea ardhini mpaka ndani ya majumba na wengine huita **(Nyota Jaha)**, kwa maana ni nyota yenye utukufu, mtu akipata bahati ya kuiona akaomba atakacho atapata, kwa hiyo watu hukesha usiku kusubiri Nyota hiyo ya uwongo ili waombe magari, nyumba, na mafanikio mbalimbali katika biashara zao n.k! wakaacha kumuomba Allaah msamaha wa madhambi yao makubwa na madogo.

DARSA YA SABA
ZAKAATUL FITRI NA SWALA YA EID MBILI

MAANA YA ZAKAATUL FITRI

Zakaatul Fitri ni: Zaka inayotolewa kwa ajili ya kuruhusiwa kula mchana.

NI IPI HUKUMU YAKE?

Zaka hii ni wajibu kwa kila muislamu, awe mdogo au mkubwa, mwanamme au mwanamke, muungwana au mtumwa, kwa hadithi ya Ibn Umar (Allaah amridhie):

«فَرَضَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ زَكَاةَ الفِطْرِ صَاعًا مِنْ تَمْرٍ، أَوْ صَاعًا مِنْ شَعِيرٍ عَلَى العَبْدِ وَالحُرِّ، وَالذَّكَرِ وَالأُنْثَى، وَالصَّغِيرِ وَالكَبِيرِ مِنَ المُسْلِمِينَ»

“Mtume ﷺ amefaradhisha Zakaatul Fitri pishi ya tende au shairi, juu ya mtumwa na muungwana, mwanamme na mwanamke, mdogo na mkubwa miongoni mwa waislamu”[95].

JE NI MWAKA GANI ILIFARADHISHWA ZAKA HIYO?

Zakaatul Fitri ilifaradhishwa katika mwezi wa Sha’bani mwaka wa pili wa hijra (tangu Mtume ﷺ kuhamia mji wa Madina).

HEKIMA YA KUFARADHISHWA KWAKE

Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbaas (Allaah amridhie) amesema:

«فَرَضَ رَسُوْلُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ زَكَاةَ الفِطْرِ طُهْرَةً لِلصَّائِمِ مِن اللَّغْوِ والرَّفَثِ وَطُعْمَةً لِلْمَسَاكِيْنِ»

“Amefaradhisha Mtume ﷺ Zakaatul Fitri kwa ajili ya kumtwaharisha mfungaji kutokana na maneno machafu na upuuzi na kwa ajili ya kuwa ni chakula kwa masikini”[96].

Na pia unatoa kwa ajili ya kushukuru neema ya Allaah juu yako kwa kutekeleza ibada mbalimbali ndani ya mwezi wa ramadhani.

Amesema sheikh Ibn Uthaymiin (Allaah amrehemu):

"وَسَبَبُهَا إِظْهَارُ شُكْرِ نِعْمَةِ اللهِ تَعَالَى عَلَى الْعَبْدِ لِلْفِطْرِ مِنْ رَمَضَانَ وَإِكْمَالِهِ"

“Sababu ya kutoa kwake (Zakaatul hiyo) ni kudhihirisha shukrani ya neema za Allaah Ta’alaa juu ya mja, kwa (kuruhusiwa) kula mchana baada ya kukamilisha kwake (funga ya) ramadhani”[97].

NI NANI INAMPASA KUTOA ZAKAATUL FITRI?

Masharti ya mtu anaewajibika kutoa Zakaatul Fitri ni mawili:

1. Awe ni muislamu.

95- Bukhari (1503), Muslim (984) na wengine.
96- Abu Daud (1609), Ibn Maajah (1827) na wengine.
97- Al-Fataawa (Jz. 18, Uk. 257).

2. Awe na chakula cha ziada baada ya chakula cha kumtosheleza yeye na familia yake mchana wa siku ya Eid na usiku wake.

JE NI WAJIBU KWA MTOTO MDOGO KUTOA ZAKAATUL FITRI?

Amesema Imam Shaukani (Allaah amrehemu):

"وُجُوبُ فِطْرَةِ الصَّغِيرِ فِي مَالِهِ... إنْ كَانَ لِلصَّغِيرِ مَالٌ، وَإِلَّا وَجَبَتْ عَلَى مَنْ تَلْزَمُهُ النَّفَقَةُ وَإِلَى هَذَا ذَهَبَ الْجُمْهُورُ"

"Inawajibika (Zakaatul) Fitri ya mtoto mdogo katika mali yake ikiwa ana yeye mali, na kama hana (mali) itamuwajibikia yule ambaye yanamlazimu yeye matumizi yake (msimamizi wake), kwa kauli waliokwenda nayo maulamaa wengi"[98].

JE MWANA WA MATUMBONI (MIMBA) HUTOLEWA ZAKAATUL FITRI?

Amesema Ibn Uthaimiin (Allaah amrehemu):

"يُسْتَحَبُّ الْإِخْرَاجُ عَنِ الْجَنِيْنِ...، وَالْإِخْرَاجُ عَنْهُ قَبْلَ نَفْخِ الرُّوْحِ فِيْهِ نَظَرٌ؛ لِأَنَّهُ لَيْسَ إِنْسَانًا، فَإِنَّمَا تُخْرَجُ عَمَّنْ نُفِخَتْ فِيْهِ الرُّوْحُ».

"Inapendekezwa kumtolea Zakaatul Fitri mwana wa matumboni (mimba), lakini kumtolea yeye kabla ya kupuliziwa roho (jambo hilo) ndani yake linahitaji kuchunguzwa, kwa sababu bado hajawa mtu, kwa hiyo itatolewa (Fitri) kwa yule ambaye amepuliziwa ndani yake roho"[99].

JE NI SHARTI MTU AWE ANAMILIKI KIWANGO MAALUMU?

Hakuna dalili yenye kufahamisha kwamba mtu anatakiwa kumiliki kiwango maalumu ili aweze kutoa Zakaatul Fitri, ndiyo maana maulamaa wanataja sharti la mtu kuwa muislamu na kupata ziada ya chakula chake yeye na familia yake mchana wa Eid na usiku wake, atatoa kiasi cha kilo 2 na nusu au kilo 3 ya chakula kinacho pendwa zaidi katika mji wake.

Amesema Imam Shaukani (Allaah amrehemu):

"وَهَذَا هُوَ الْحَقُّ؛ لِأَنَّ النُّصُوصَ أُطْلِقَتْ وَلَمْ تَخُصَّ غَنِيًّا وَلَا فَقِيرًا"

"Hii ndio sawa, kwa sababu maandiko ya kisheria yameachiliwa, wala hazijamhusisha tajiri au masikini"[100].

JE ITAFAA KUTOA KIASI CHA PESA BADALA YA CHAKULA?

Ama kuhusu kutoa pesa badali ya chakula jambo hili hakuna aliye ruhusu katika maimamu wanne (Allaah awarehemu) isipokuwa Abu Hanifa pekee.

Amesema sheikh Ibn Baaz Allaah amrehemu:

98- Nailul Autwwari (Jz. 4, Uk. 214).

99- Fataawa warasaail (Jz 6, Uk. 616) Ibn Uthaimin.

100- Nailul Autwaar (Jz. 4, Uk. 251).

"وَالصَّوَابُ أَنَّ الْوَاجِبَ إِخْرَاجُهَا طَعَامًا عِنْدَ جُمْهُوْرِ أَهْلِ الْعِلْمِ"

“Kauli ya maulamaa wengi ni kwamba, wajibu ni kutoa chakula, na hiyo ndio kauli sahihi”[101].

Amesema sheikh Ibn Uthaymiin Allaah amridhie:

"الصَّحِيْحُ أَنَّهُ لَا يَجُوْزُ إِخْرَاجُ الْقِيْمَةِ مِنَ الطَّعَامِ فِيْ زَكَاةِ الْفِطْرِ"

“Kauli sahihi ni kwamba haifai katika Zakaatul Fitri kutoa kiasi cha pesa badali ya chakula”[102].

NI WAKATI GANI ITATOLEWA ZAKAATUL FITRI?

Kauli yenye nguvu ni kwamba wakati wa wajibu wa kutoa Zakaatul Fitri ni baada ya kuzama jua siku ya mwisho ya ramadhani na wakati bora zaidi ni asubuhi ya siku ya Eid, na lau kama mtu atasilimu au atazaliwa mtoto siku ya mwisho ya Ramadhani kabla ya kuzama jua kwa muda mchache ni wajibu wake kutoa zakaatul fitri, na haifai kutoa baada ya swala ya Eid, kwa hadithi.

«فَرَضَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ زَكَاةَ الفِطْرِ... وَأَمَرَ بِهَا أَنْ تُؤَدَّى قَبْلَ خُرُوجِ النَّاسِ إِلَى الصَّلاَةِ»

“Amefaradhisha Mtume ﷺ Zakaatul fitri... Na ameamrisha itolewe kabla watu hawajatoka kwenda kuswali”[103].

MAMBO MBALIMBALI KUHUSU ZAKAATUL FITRI:

1) Hapewi Zakaatul fitri isipokuwa masikini tena aliye muislamu.
1) Inafaa kumfanya mtu wakala kwa ajili ya kutoa Zakaatul fitri.
2) Inafaa kwa masikini kuwakilishwa katika Zakaatul fitri.
3) Hakuna dua maalumu ya kusoma wakati wa kutoa.
4) Zakaatul fitri hutolewa katika sehemu ambayo itakupata sikukuu ya Iddi hata kama ni mbali na mji wako.
5) Inajuzu kumtolea Zakaatul fitri mtumishi wako wa ndani akiwa ni muislamu na asili ni kuwa atoe yeye mwenyewe.
6) Haifai kumpatia mtumishi wako ila akiwa ni masikini.
7) Inafaa kwa mtu aliyepewa Zakaatul fitri kutoa kumpa mtu mwingine ambaye anastahiki na pia anaruhusiwa kuuza alichopewa.
8) Akichelewa kutoa Zakaatul fitri kwa udhuru au kwa sababu ya kukosa masikini wa kumpatia hakuna ubaya, na atatoa wakati akipata wepesi wa hilo.
9) Itafaa kumpa Zakaatul fitri masikini mmoja hata kama ni chakula cha watu wengi.

101- Al-Fataawa (Jz. 15, Uk. 287).
102- Al-Fataawa (Jz. 18, Uk. 265).
103- Bukhari (1503) na Muslim (986).

10) Mwenye kutoa Zakaatul fitri baada ya swala ya Iddi, haitazingatiwa na itakuwa ni sawa na sadaka nyingine.
11) Akichelewa kutoa Zakaatul Fitri kwa makusudi, atapata dhambi na itamlazimu yeye kulipa.
12) Itafaa kumpatia msimamizi wa Zakaatul fitri kwa siku moja au mbili kabla ya kumalizika ramadhani.

SWALA YA EID MBILI:

KUITWA KWAKE EID

Imeitwa swala ya Eid kwa jina hilo kwa sababu kujirejea kwa kwa neema ambazo Allaah amewapa waja wake, ambazo ni kutekeleza ibada mbalimbali katika siku hiyo.

HUKUMU YAKE

Kuna khilafu baina ya Maulamaa kuhusu hukumu ya swala ya Eid na kauli iliyo na nguvu ni kwamba hukumu yake ni wajibu, mpaka Mtume ﷺ aliwaamrisha wanawake wenye hedhi kuhudhuria katika viwanja vya kuswalia swala ya Eid, kwa hadithi ya Ummu ‘Atwiyya (Allaah amridhie):

«أَمَرَنَا - تَعْنِي النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - أَنْ نُخْرِجَ فِي الْعِيدَيْنِ، الْعَوَاتِقَ، وَذَوَاتِ الْخُدُورِ، وَأَمَرَ الْحُيَّضَ أَنْ يَعْتَزِلْنَ مُصَلَّى الْمُسْلِمِينَ»

“Ametuamrisha (anakusudia Mtume ﷺ tuwatoe wanawake baleghe (vigori) na wanawake bikra (wana wari) waliostiriwa majumbani katika (kuhudhuria swala ya) Eid mbili, na akawaamrisha wanawake wenye hedhi kujitenga na mahala pa kuswali waislamu”[104].

KUOGA NA KUJIPAMBA KWA AJILI YA SWALA YA EID

Imepokewa kutoka kwa baadhi ya Maswahaba akiwemo Ibn Umar (Allaah amridhie), kwamba walikuwa wanaoga siku ya Eid kabla ya kwenda kuswali na pia hapana vibaya kuoga kabla au baada ya swala ya alfajri.

Amesema Imam Nnawawi (Allaah amrehemu):

"قَالَ الشَّافِعِيُّ وَالْأَصْحَابُ يُسْتَحَبُّ الْغُسْلُ لِلْعِيدَيْنِ وَهَذَا لَا خِلَافَ فِيهِ، وَالْمُعْتَمَدُ فِيهِ أَثَرُ ابْنِ عُمَرَ وَالْقِيَاسُ عَلَى الْجُمُعَةِ، وَفِي وَقْتِ صِحَّةِ هَذَا الْغُسْلِ قَوْلَانِ مَشْهُورَانِ: (أَحَدُهُمَا) بَعْدَ طُلُوعِ الْفَجْرِ نَصَّ عَلَيْهِ فِي الْأُمِّ (وَأَصَحُّهُمَا) بِاتِّفَاقِ الْأَصْحَابِ يَجُوزُ بَعْدَ الْفَجْرِ وَقَبْلِهِ"

“Amesema Imam Shaafi’ na maulamaa wakubwa wa fiqhi (katika madhebu) kwamba inapendekezwa kuoga kwa ajili ya Eid mbili na hili halina khilafu yoyote ndani yake, na mategemeo katika hilo ni athari ya Ibn Umar na kwa kupigia kiasi siku ya Ijumaa. Na kuhusu wakati sahihi wa kuoga kuna kauli mbili zenye nguvu:

104- Bukhari (980) na Muslim (890).

(moja yao) ni kwamba baada ya kuchomoza alfajri, amelitaja wazi hilo (imam shaafi') katika kitabu Al-Ummu, na iliyo sahihi zaidi (katika kauli mbili hizo) kwa makubaliano ya maulamaa wakubwa inafaa baada ya alfajiri na kabla yake"[105].

SUNNA KATIKA EIDIL FITRI NI KULA TENDE KABLA YA KWENDA KUSWALI

Kutoka kwa Anas (Allaah amridhie) amesema:

«كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لاَ يَغْدُو يَوْمَ الفِطْرِ حَتَّى يَأْكُلَ تَمَرَاتٍ، وَيَأْكُلُهُنَّ وِتْرًا»

"Alikuwa Mtume ﷺ haondoki (kweye kuswali) siku ya Eidil Fitri mpaka ale tende na akila kwa witri"[106].

Ama swala ya Eidil Adh-ha kwa hadithi ya Buraida kutoka kwa baba yake (Allaah amridhie) amesema:

«وَلَا يَطْعَمُ يَوْمَ الأَضْحَى حَتَّى يُصَلِّيَ»

"Na hali chochote siku ya Eidil Adh-ha mpaka amalize kuswali"[107].

Amesema Ibn Hajar (Allaah amrehemu):

"قَالَ الْمُهَلَّبُ: الْحِكْمَةُ فِي الْأَكْلِ قَبْلَ الصَّلَاةِ أَنْ لَا يَظُنَّ ظَانٌّ لُزُومَ الصَّوْمِ حَتَّى يُصَلِّيَ الْعِيدَ فَكَأَنَّهُ أَرَادَ سَدَّ هَذِهِ الذَّرِيعَةِ. وَقَالَ غَيْرُهُ لَمَّا وَقَعَ وُجُوبُ الْفِطْرِ عَقِبَ وُجُوبِ الصَّوْمِ اسْتُحِبَّ تَعْجِيلُ الْفِطْرِ مُبَادَرَةً إِلَى امْتِثَالِ أَمْرِ اللَّهِ تَعَالَى "

"Amesema Al-Muhallab: Hekima ya kula kabla ya kuswali ili asije akadhani mwenye kudhani kwamba ni lazima mtu kujizuilia (kula) mpaka amalize kuswali Eid, kana kwamba (Mtume ﷺ) ametaka kuifunga njia hii. Na wengine wamesema: wakati ulipokuja wajibu wa kula baada tu ya kumalizika ibada ya kufunga ikapendekezwa kufanya haraka kula kwa ajili ya kuharakisha kutekeleza amri ya Allaah Ta'alaa"[108].

SUNNA NI KUSWALI SWALA YA EID VIWANJANI

Kutoka kwa Abu Said (Allaah amridhie) amesema:

«كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَخْرُجُ يَوْمَ الفِطْرِ وَالأَضْحَى إِلَى المُصَلَّى»

"Alikuwa Mtume ﷺ anatoka siku ya Eidil Fitri na Eidil Adh-ha kwenda katika Muswalla (kiwanja cha kuswalia)"[109].

Amesema Ibn Hajar (Allaah amrehemu):

"وَفِيهِ الْخُرُوجُ إِلَى الْمُصَلَّى فِي الْعِيدِ وَأَنَّ صَلَاتَهَا فِي الْمَسْجِدِ لَا تَكُونُ إِلَّا عَنْ ضَرُورَةٍ"

"Kuna katika hadithi hii (kwamba sunna) ni kutoka kwenda kiwanjani kuswali siku ya Eid na haipasi kuswali msikitini ila kwa dharura". [Al-Fat-hu (Jz.2, UK. 450)].

105- Al-Majmuu' (Jz. 5, Uk. 7).
106- Bukhari (953). Akila kwa idadi ya witri, tende 1, 3, 5,7 n.k.
107- Sunan Tirmidh (542).
108- Fat-hul baari (Jz. 2, Uk. 447).
109- Bukhari (956) na Muslim (890).

Na sehemu nyingine amesema:

"وَاسْتُدِلَّ بِهِ عَلَى اسْتِحْبَابِ الْخُرُوجِ إِلَى الصَّحْرَاءِ لِصَلَاةِ الْعِيدِ وَأَنَّ ذَلِكَ أَفْضَلُ مِنْ صَلَاتِهَا فِي الْمَسْجِدِ لِمُوَاظَبَةِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى ذَلِكَ مَعَ فَضْلِ مَسْجِدِهِ".

“Na wametolea dalili kwa hadithi sunna ya kutoka kwenda kwenda majangwani (nje ya mji) kwa ajili ya swala ya Eid na kwamba hilo ndio bora zaidi kuliko kuswalia msikitini, kwa sababu ya kudumu kwake Mtumeﷺ juu ya jambo hilo, pamoja na fadhila za msikiti wake”[110].

SUNNA NI KWENDA VIWANJANI KWA MIGUU (BILA KUPANDA KIPANDO)

Imepokewa kutoka kwa Ally (Allaah amridhie) amesema:

«مِنَ السُّنَّةِ أَنْ تَخْرُجَ إِلَى العِيدِ مَاشِيًا»

“Miongoni mwa sunna ni kutoka kwenda kwenye swala ya Eid kwa

SUNNA YA KUBADILISHA NJIA WAKATI WA KURUDI

Imepokewa kutoka kwa Abu Huraira (Allaah amridhie) amesema:

«كَانَ يَأْتِي الْعِيدَ مَاشِيًا، وَيَرْجِعُ فِي غَيْرِ الطَّرِيقِ الَّذِي ابْتَدَأَ فِيهِ»

“Alikuwa (Mtumeﷺ) anaenda kwenye swala ya Eid kwa kutembea (kwa miguu) na anarudi kwa isiyo kuwa njia ambayo alikuja nayo”[112].

Amesema Imam Shaafi’ (Allaah amrehemu):

"الْإِتْيَانُ مِنْ طَرِيقٍ غَيْرِ الَّتِي غَدَا مِنْهَا... فَأُحِبُّ ذَلِكَ لِلْإِمَامِ، وَالْعَامَّةِ"

“Napendelea kwa imamu na watu wengine kurudi na njia (nyingine) tafauti na njia ambayo alienda nayo”[113].

WAKATI WA SWALA YA EID

Wakati wa swala ya Eid ni: baada ya kupanda jua kiasi cha urefu wa upinde tangu kuchomoza kwake, tafauti na baadhi ya maimamu wanavyofanya, wanachelewa sana kwenda viwanjani kuswali Eid mpaka jua linakuwa kali.

Imam Bukhari ameweka mlango katika sahihi yake, akasema:

"بَابُ التَّبْكِيرِ إِلَى العِيدِ"

“Huu ni mlango wa kurauka mapema kwenda kuswali Eid”[114].

110- Fat-hul baari (Jz. 2, Uk. 450).

111- Sunan Tirmidh (530). Anakusudia Eidil Fitri ambayo imethibiti ndani kula kabla ya swala.

112- Sunan Ibn Maajah (1300).

113- Al-Ummu (Jz. 1, Uk. 267).

114- Bukhari (Jz. 2, Uk. 19).

Halafu chini yake akataja maneno ya Swahaba Abdullaahi Bin Busri (Allaah amridhie) wakati alipoenda kuswali Eidil Fitri au Eidil Adh-ha akachukia kuchelewa kwa imam akasema:

"إِنْ كُنَّا فَرَغْنَا فِي هَذِهِ السَّاعَةِ وَذَلِكَ حِينَ التَّسْبِيحِ"

“Hakika sisi tulikuwa wakati huu tumeshamaliza (kuswali), nao ni wakati wa Tasbiih (mwanzo wa swala ya dhuha)”[115].

Na mwanzo wa swala ya dhuha ni baada ya kupanda jua kiasi cha upinde, na baadhi ya maulamaa wamekadiria wakasema ni kiasi cha dakika 13 tangu kuchomoza kwa jua.

NAMNA YA KUSWALI SWALA YA EID:

Swala ya Eid ni rakaa mbili, utasoma Takbira saba katika rakaa ya kwanza baada ya Takbira ya kuhirimia (Takbiratul ihram) na dua ya kufungulia swala, kasha katika rakaa ya pili utasoma Takbira tano katika baada ya kunyanyuka kutoka kwenye sijda ya pili, wala haingii katika hizo Takbira ya kwenda kurukuu, kama ilivyokuja katika hadithi.

Imepokewa na Aisha (Allaah amridhie) amesema:

«كَبَّرَ فِي الْفِطْرِ وَالْأَضْحَى سَبْعًا وَخَمْسًا، سِوَى تَكْبِيرَتَيِ الرُّكُوعِ»

“(Mtume ﷺ alipiga Takbira saba katika Eidil Fitri na Takbira tano katika Eidil Adh-ha zisizo kuwa Takbira mbili za kurukuu”[116].

KISOMO KATIKA SWALA YA EID

Utasoma kwa kudhihirisha sauti, katika rakaa ya kwanza baada ya surat Al-faatiha utasoma surat Al-a’laa (Sabbihisma) na rakaa ya pili utasoma suratul Ghaashiyah kwa hadithi ya Nu’maan Bin Bashir (Allaah amridhie) amesema:

«كَانَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْرَأُ فِي الْعِيدَيْنِ، وَفِي الْجُمُعَةِ بِسَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى، وَهَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ»، قَالَ: «وَإِذَا اجْتَمَعَ الْعِيدُ وَالْجُمُعَةُ، فِي يَوْمٍ وَاحِدٍ، يَقْرَأُ بِهِمَا أَيْضًا فِي الصَّلَاتَيْنِ».

“Mtume ﷺ alikuwa anasoma (suratul ‘Alaa) na (suratul Ghaashiya) katika Eid mbili na siku ya Ijumaa, Amesema (Nu’maan): “Na ikikusanyika Eid na Ijumaa katika siku moja anazisoma sura zote hizo katika swala zote mbili”[117].

Na katika riwaya nyingine Umar alimuuliza Abu Waaqid Al-Laythi (Allaah awaridhie) kuhusu kisomo cha Mtume ﷺ katika Eid mbili akasema:

«كَانَ يَقْرَأُ فِيهِمَا بِـ {ق وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ} و {اقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَانْشَقَّ الْقَمَرُ}»

“Alikuwa anasoma katika rakaa mbili hizo (surat Qaaf) na (surat Al-Qamar”[118].

115- Abu Daud (1135), Ibn Majah (1317) na wengine.
116- Sunan Ibn Majah (1280).
117- Muslim (878).
118- Muslim (891).

TAKBIRA ZA EID NA WAKATI WAKE

Imesuniwa kuleta Takbira katika sikukuu za Eid mbili na imekokotezwa zaidi katika Eidil fitri kwa kauli yake Allaah:

﴿وَلِتُكۡمِلُواْ ٱلۡعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُواْ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمۡ وَلَعَلَّكُمۡ تَشۡكُرُونَ﴾

“Na mtimize hiyo hisabu na mumtukuze Allaah kwa kuwa amekuongoeni ili mpate kumshukuru”(119).

Hakuna hadithi sahihi inayo fahamisha mwanzo na mwisho wa Takbira isipokuwa imepokewa kutoka kwa baadhi ya Maswahaba (Allaah awaridhie) kwamba wao walikuwa wanaleta Takbira wakati wa kuelekea kwao viwanjani na mwisho wake katika Eidil Fitri ni pale atakapokuja imam kiwanjani kwa ajili ya swala. Ama kuhusu Eidil Adh-ha amesema Ibn Hajar (Allaah amrehemu):

"وَأَصَحُّ مَا وَرَدَ فِيهِ عَنِ الصَّحَابَةِ قَوْلُ عَلِيٍّ وَابْنِ مَسْعُودٍ إِنَّهُ من صبح يَوْمِ عَرَفَةَ إِلَى آخِرِ أَيَّامِ مِنَى"

“Kauli sahihi iliyokuja kutoka kwa Maswahaba kuhusiana (na Takbira za Eidil mbili) ni kauli ya Ali na Ibn Masoud (Allaah awaridhie) kwamba (Takbira) ni kuanzia asubuhi ya siku ya Arafa mpaka mwisho wa siku za (kukaa) Mina (wakati wa alasiri siku ya tarehe 13 Dhul-hijjah)](120).

MATAMKO YA TAKBIIRA

Ama matamko ya Takbira yaliyopokewa kwa Maswahaba (Allaah awaridhie) ni:

اللهُ أَكْبَرُ ** اللهُ أَكْبَرُ ** اللهُ أَكْبَرُ ** كَبِيْرًا

“Allaahu Akbar Allaahu Akbar Allaahu Akbar kabiira”(121).

اللهُ أَكْبَرُ اللهُ أَكْبَرُ لَا إِلهَ إِلَّا االلّٰه وَاللهُ أَكْبَرُ، اللهُ أَكْبَرُ وَلِلَّهِ الحَمْدُ

“Allaahu Akbar Allaahu Akbar Laa ilaaha illaLlaahu wallaahu Akbar Allaahu Akbar walillaahil hamdu”(122).

Na haifai kuongeza maneno zaidi ya hayo katika Takbira kama wanavyofanya hilo baadhi ya watu, huo ni uzushi katika dini.

MAAMUMA HANYANYUI SAUTI KWA KUITIKIA TAKBIRA:

Amesema Imam Nnawawi (Allaah amrehemu):

"وَأَمَّا غَيْرُ الْإِمَامِ فَالسُّنَّةُ الْإِسْرَارُ بِالتَّكْبِيرِ سَوَاءٌ الْمَأْمُومُ وَالْمُنْفَرِدُ وَأَدْنَى الْإِسْرَارِ أَنْ يُسْمِعَ نَفْسَهُ إِذَا كَانَ صَحِيحَ السَّمْعِ ... وَهَذَا عَامٌّ فِي الْقِرَاءَةِ وَالتَّكْبِيرِ وَالتَّسْبِيحِ فِي الرُّكُوعِ وَغَيْرِهِ وَالتَّشَهُّدِ وَالسَّلَامِ وَالدُّعَاءِ سَوَاءٌ وَاجِبُهَا وَنَفْلُهَا"

119- Surat Al-Baqara/185.
120- Fat-hul baari (Jz. 2, Uk. 462).
121- Al-Muswannaf (Jz. 2, Uk. 168).
122- Angalia kitabu: As sharhul mumti’ (Jz. 5, Uk. 227).

“Ama asiyekuwa imam, sunna ni kufanya siri (kuficha) takbira, ni sawa awe maamuma au mwenye kuswali peke yake, na uchache wa kuficha ni kujisikilizisha yeye mwenyewe akiwa anasikia vizuri… na hukumu hii ni yenye kuenea katika kisomo, takbira, tasbiih katika rukuu na sehemu nyingine, na katika tashahud na (wakati wa kutoa) salam, na wakati wa kuomba dua, sawa iwe ni swala ya faradhi au sunna”[123].

HAKUNA KATIKA VIWANJA VYA EID SUNNAH SI KABLA WALA BAADA YA SWALA:

Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas (Allaah amridhie) amesema:

«خَرَجَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَوْمَ فِطْرٍ، فَصَلَّى رَكْعَتَيْنِ لَمْ يُصَلِّ قَبْلَهُمَا وَلَا بَعْدَهُمَا»

“Mtume ﷺ alitoka siku ya Eidil Fitri, akaswali rakaa mbili (za Eid), wala hakuswali kabla yake wala baada yake”[124].

Amesema Imam Zuhri (Allaah amrehemu):

"لَمْ أَسْمَعْ أَحَدًا مِنْ عُلَمَائِنَا يَذْكُرُ أَنَّ أَحَدًا مِنْ سَلَفِ هَذِهِ الْأُمَّةِ كَانَ يُصَلِّي قَبْلَ تِلْكَ الصَّلَاةِ وَلَا بَعْدَهُ"

“Sijamsikia yeyote katika maulamaa wetu akitaja kwamba kuna katika Salaf wa umma huu alikuwa anaswali kabla ya swala hiyo (ya Eid) wala baada yake”[125].

KUPEANA PONGEZI BAADA YA SWALA YA EID:

Amesema Imam Ahmad (Allaah amrehemu):

"وَلَا بَأْسَ أَنْ يَقُولَ الرَّجُلُ لِلرَّجُلِ يَوْمَ الْعِيدِ: تَقَبَّلَ اللَّهُ مِنَّا وَمِنْك"

“Hapana vibaya kwa mtu kumwambia mwenzie siku ya Eid: Allaah atutakabalie sisi na wewe”[126].

TANBIH:

1. Mwisho wa kuswali Eid ni wakati wa kupondoka jua na hapo utakuwa umeingia wakati wa adhuhuri.
2. Endapo mtu hakujua kwamba hiyo ni siku ya Eid isipokuwa baada ya kumalizika wakati wake, ataswali siku inayofuata kama alivyoswali imam, na kauli ya wengi katika maulamaa ni kwamba ataswali bila ya khutba hata ikiwa ni jamaa.
3. Endapo watu wataswali msikitini kwa dharura ya mvua n.k basi ataswali Tahiyyatul masjid kama ilivyo kawaida.
4. Wanawake ni haramu kujipaka manukato wakati wa kutoka nje ya nyumba zao, na vilevile ni lazima kuvaa mavazi ya sitara, ni sawa ametoka kwa ajili ya swala au jambo lingine.
5. Hakuna dua maalumu baina ya Takbira katika swala ya Eid.

123- Al-Majmuu’ (Jz. 3, Uk. 295).
124- Sunan Abi Daud (1159).
125- ‘Aunul ma’buud (Jz. 4, Uk. 16).
126- Al-Mughni (Jz. 2, Uk. 295).

6. Haijathibiti kuleta Takbira katika viwanja vya Eid au misikitini kwa sauti ya pamoja.
7. Takbira za Eid ni sunna endapo mtu akisahau kusoma ndani ya swala hakuna juu yake sijda ya kusahau.
8. Haijathibiti katika viwanja vya Eid kuhutubu juu ya mimbari.
9. Khutba ya Eid ni moja tu na wala haifunguliwi kwa Takbira, inaanza kwa kumhimidi Allaah na hiyo ndiyo sunna.
10. Kusikiliza khutba ni sunna wala si wajibu, isipokuwa ni vizuri muislamu kubaki kwa ajili ya kupata faida.
11. Haijathibiti kuhusisha siku ya Eid na kuzuru makaburi, hiyo ni bidaa, kama mtu anataka kuzuru basi aende siku yoyote lakini asihusishe siku ya Eid siku fulani.
12. Miongoni mwa bidaa ni dhana ya baadhi ya watu kwamba ni sunna kuswali usiku wa kuamkia siku ya Eid.
13. Miongoni mwa makosa ni kauli ya baadhi ya maimamu: Mwenye kumuasi Allaah siku ya Eid ni sawa amemuasi Allaah siku ya kiama.
14. Kunyanyua mikono kwa kila Takbira jambo hilo lina khilafu baina ya Maulamaa.

UDHAIFU WA HADITHI KUHUSIANA NA FADHILA ZA KUHUISHA USIKU YA EID:

Amesema Imam Nnawawi (Allaah amrehemu):

"وَاحْتَجَّ لَهُ أَصْحَابُنَا بِحَدِيثِ أَبِي أُمَامَةَ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ "مَنْ أَحْيَا لَيْلَتَيْ الْعِيدِ لَمْ يَمُتْ قَلْبُهُ يَوْمَ تَمُوتُ الْقُلُوبُ" وَفِي رِوَايَةِ الشَّافِعِيِّ وَابْنِ مَاجَهْ "مَنْ قَامَ لَيْلَتَيْ الْعِيدَيْنِ مُحْتَسِبًا لِلَّهِ تَعَالَى لَمْ يَمُتْ قَلْبُهُ حِينَ تَمُوتُ الْقُلُوبُ". وَأَسَانِيدُ الْجَمِيعِ ضَعِيفَةٌ"

“Wametolea hoja hilo maulamaa wetu (kishafi) kwa hadithi ya Abu Umama kutoka kwa Mtume ﷺ: (Mwenye kuhuisha nyusiku mbili za Eid hautakufa moyo wake siku ambayo itakufa mioyo). Na katika riwaya ya Imam Shafi’ na Ibn Majah: (Mwenye kusimama (kuswali usiku) wa Eid mbili hali ya kutarajia malipo kutoka kwa Allaah Ta’laa, hautakufa moyo wake wakati itapokufa mioyo). Na sanadi za (wapokezi) wote ni dhaifu”.

Wallaahu A’alam.
Ijumaa 29/sha’bani/1443H – 1/4/2022M.
Pongwe Tanga.